# Nipashe

Alhamisi Machi 5, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580171

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Wagonjwa wanaume, wanawake, watoto wanavyolala wodi moja

UKURASA 3




UKURASA 13

# Maalim Seif aeleza kilichompeleka Ikulu

• **Agusia** mbio za urais uchaguzi mkuu wa 2020, hatima ya Ukawa...*Endelea ukurasa 2*



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipokea tuzo ya kukumbukwa na kutambua mchango wake, kwa kusaidia na kuwezesha wanawake na watoto, pia kuwa mwanamke wa kwanza nchini kushika nafasi ya juu ya uongozi ya Makamu wa Rais, kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), Mary Rusimbi, baada ya kufungua kongamano la kuadhimisha na kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani na Miaka 25, baada ya mkutano wa Beijing, lililofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

## YALIYOMO


UKURASA WA 8

**CHADEMA YAJITOSA SAKATA LA LEMA**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimetangaza...

UKURASA WA 25

**WAFUNGWA 54,000 WAACHIWA KUEPUKA MAAMBUKIZI CORONA**

IRAN imewaachia huru kwa muda wafungwa zaidi ya 54,000 ikiwa ni...


## Raia wa Cameroon apigwa faini mil. 100/-

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Abiria wakwama siku tatu daraja la Morogoro

• **Madereva** wa malori watoa kilio, Majaliwa aja juu... *Ukurasa 2*


**MICHEZO** RAIS CAF AFUATA DABI SIMBA, YANGA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Abiria wakwama siku 3 daraja la Morogoro

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

NI mkwamo! Ndicho kinachoweza kuelezwa na watumiaji wa barabara ya Morogoro hadi Dodoma ambao wanasota kwa siku ya tatu sasa tangu daraja la eneo la Kiegeya, maarufu kama daraja la Mkange, Wilaya ya Gairo kuzolewa na maji.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alitembelea eneo hilo na kuonyesha kutoridhishwa na utendaji kazi wa wataalamu, ambao walishindwa kutengeneza njia mbadala za kubeba magari yenye uwezo wa tani 30 hadi 40, ili kupunguza msongamano.

Nipashe ilishuhudia malori yakiwa yamesimama pande zote mbili huku kukiwa hakuna huduma za vyakula wala vyoo.

Kutokana na ahadi iliyotolewa juzi na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe na Naibu Waziri wa Ujenzi, kuwa juzi saa nne usiku barabara hiyo ingeanza kupitisha gari moja moja, baadhi ya mabasi yalikata tiketi kwa abiria ambao wamekwama eneo hilo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya madereva wa malori ya mizigo na magari ya mafuta, walisema usalama wao uko shakani kutokana na mali walizobeba.

"Hadi sasa hatuna uhakika wa usalama kwa kuwa magari yamebeba mafuta, hapa hakuna gari la zimamoto na ikitokea jambo lolote kama kuibiwa mafuta hatutaweza kuzuia, lakini pia hatuwezi kuzunguka kutokana na umbali pamoja na kwamba matajiri wetu wameona mkwamo lakini wamekaa kimya," alisema.

**PM ATOA AGIZO**

Jana Waziri Mkuu, alipotembelea eneo hilo pamoja na kuwapa pole watumiaji wa barabara, alisema hajaridhishwa na utendaji kazi wa wataalamu.

Alimwagiza Mkuu wa Majeshi na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), mikoa wa Dodoma na Morogoro kushirikiana kuleta wataalamu wafanye kazi usiku na mchana kuhakikisha kazi hiyo inamalizika ifikapo leo jioni na gari la kwanza kupita ili kuondoa msongamano na hali ngumu iliyopo.

Alisema ni uzembe mkubwa kwa Tanroads kutokagua madaraja hayo mara kwa mara, wangefanya hivyo, athari zingejulikana mapema na hatua za kunusuru zingechukuliwa.

Waziri Mkuu alimtaka Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Patrick Mfugale, kuondoka na Kaimu Meneja wa wakala huyo mkoani Morogoro kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wake kwa kuwa serikali inatoa fedha kwa ajili ya ukaguzi wa madaraja ya barabara hiyo ya kimataifa.

Alishangazwa na wataalamu hao kushindwa kutengeneza njia mbadala za muda mfupi, na kuwaagiza kufanya hivyo ili magari madogo yaendelee kupita. Pia, aliwataka watumiaji wa barabara kuwa wavumilivu wakati serikali inafanya jitihada mbalimbali za kurejesha mawasiliano.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, barabara hiyo ni ya kimataifa na mara kwa mara wanapokea simu kutoka kwa viongozi wa nchi jirani kuhusu watu wao kukwama katika eneo hilo.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ukarabati wa daraja la Mto Kiegeya maarufu daraja la Mkange, ambalo lilizolewa na maji na kusababisha kukatika kwa mawasiliano ya Barabara ya Morogoro-Dodoma, wilayani Gairo, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Maalim Seif aeleza kilichompeleka Ikulu

**Na Romana Mallya**

MWANASIASA mkongwe Maalim Seif Sharif Hamad, ametaja sababu za kwenda kwake Ikulu jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo na Rais John Magufuli.

Juzi, Maalim Seif (76), ambaye aliwahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alikwenda Ikulu na kuteta na Rais Magufuli. Mbali na Maalim Seif, viongozi wengine waliotinga Ikulu juzi na kuzungumza na Rais, ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, na Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia.

Haikuelezwa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu sababu hasa za viongozi hao kwenda Ikulu, ingawa watatu hao kwa pamoja katika kauli zao baada ya kutoka Ikulu, waligusia suala la uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Lakini, jana Maalim Seif alisema jijini Dar es Salaam kuwa kilichompeleka Ikulu ni matatizo ya kisiasa visiwani Zanzibar na umuhimu wa maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Alisema maridhiano hayo yalifikiwa mwaka 2010, wakikubaliana kwamba chama kinachopata kura nyingi za urais, kitaongoza nchi na kingine kitatoa Makamu wa Kwanza wa Rais na mawaziri watagawana kulingana na uwiano wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Maalim Seif alisema nia yake ya kuzungumza na Rais Magufuli ni ya muda mrefu, akibainisha kuwa kabla ya kuitwa Ikulu juzi, aliandika barua mara tatu kumwomba wazungumze, lakini hakufanikiwa.

Alisema alipata matumaini ya kufanikisha azma yake hiyo Novemba 12 mwaka jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu cha Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa cha 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudio Langu), aliposalimiana na Rais Magufuli kisha kiongozi huyo wa nchi kumpa ahadi ya kuzungumza naye.

"Wakati bado niko CUF, kulipozuka mgogoro, nilimwandikia Rais Magufuli barua ya kuomba kuonana naye na sikupata jibu. Niliandika barua ya ukumbusho mara ya kwanza, ya pili na tatu, lakini sikupata jibu. "Wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Rais Mkapa, niliposalimia na Rais Magufuli, alisema 'nasikia unanitafuta' na akaniahidi atatafuta muda tukutane.

"Jana (juzi) saa mbili asubuhi, nikapata simu kutoka kwa Katibu wake ambaye aliniambia Rais angependa kukutana nami saa 3:30 asubuhi, nikamwambia ni vizuri na hicho ndicho chanzo cha kukutana.

"Baada ya kukutana, alinitaka nimweleze niliyokusudia kumweleza. Niliona ni fursa adhimu, nikazungumza yote ya moyoni, zaidi ni suala zima la Zanzibar na mwelekeo wake.

"Zanzibar tuna matatizo na mengine ni ya kihistoria, ilifikia hatua watu hawasemezani, hawazikani hata ndugu kwa ndugu. Bahati nzuri, Rais Mzee Abeid Amani Karume alifikia mahali akasema 'hatuwezi kwenda hivyo hivyo', tukakutana naye, tukazungumza ili tumalize, nilikubali.

"Nikasema hili suala la maridhiano lisiishie kwa Maalim Seif na Karume, tukalipeleka Baraza la Wawakilishi, wote wakakubali CCM na CUF, tukasema haitoshi tukafanya kura ya maoni na asilimia 66 wakasema wanataka maridhiano," alifafanua.

Maalim Seif alisema walitoa idhini Katiba ya Zanzibar ifanyiwe marekebisho ili wafanye kazi pamoja na uchaguzi unaofuata kusiwe na mshindi na aliyeshindwa, bali wote wafanye kazi katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Maalim Seif alikumbusha kuwa baada ya uchaguzi hayo, chama chake kilikuwa na Makamu wa Kwanza wa Rais na mawaziri saba kwenye Baraza la Mawaziri na CCM walikuwa na mawaziri tisa.

Alisema uchaguzi wa mwaka 2015 ulifanyika shwari na CUF ilishinda, lakini kukaibuka matatizo tena, ambayo anaamini ni kutokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokukubali "Dhamira yangu ilikuwa nikutane na Rais Magufuli kwa sababu ni Rais wa Tanzania, na ni lazima aingilie mambo yote yatayojitokeza. Ninashukuru katika mazungumzo ilifika mahali akanielewa na mimi nimemwelewa, hicho ndicho kiini cha mazungumzo yetu," alisema kwa msisitizo.

**UKAWA MPYA**

Alipoulizwa kama kuna jitihada zozote za upinzani kuwa na umoja kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu uliopita kulipoiundwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) na kusimamisha mgombea mmoja wa urais, Maalim Seif alidokeza kuwa mazungumzo yanaendelea na yamefika patamu.

Alisema ACT-Wazalendo wanaamini katika ushirikiano kwa sababu hawawezi kwenda kwenye uchaguzi mkuu wakiwa chama kimoja kimoja na wakataraji kufanya vizuri.

"Uchaguzi 2015 kuna maeneo tulipoteza kwa kura chache sana kwa sababu kura za upinzani ziligawanyika (kwa wapinzani wenyewe). Endapo tungeungana maeneo yale, CCM ingepoteza, tunaamini vyama ambavyo vipo makini, kuungana au kushirikiana ni muhimu sana," alisema.

Maalim Seif alisema ACT-Wazalendo wanajitahidi kuafikiana hilo na mwitikio walioupata siyo mbaya, lakini wanaona ni mapema kusema wamefikia hatua gani.

"Matumaini yetu bila kupoteza muda, tukae tuangalie namna ya kuwa na ushirikiano ambao kila mmoja ataridhika," alisema. Kuhusu hatima yake kisiasa na uongozi na kama amepanga kuwania tena urais mwaka huu, Maalim Seif alisema yeye ni mwanasiasa na analoliangalia ni kama bado wananchi wa imani naye.

"Mara zote nilizogombea niliamini wananchi wana imani na mimi ndiyo maana nikashinda, nimesema mara nyingi, wakati wowote nikiona imani ya wananchi imepotea sitoendelea, uchunguzi tunaofanya Zanzibar, bado wananchi wana imani na mimi, wanasubiri uamuzi wangu kama nitagombea ama sitagombea," alisema.

Maalim Seif alisema wadau, wanachama na wafuasi wake ambao wameanza kumshinikiza kugombea na anaamini mwaka huu ule atashinda.

Alitamba kuwa mwaka huu CCM watashindwa vibaya na upinzani umejipanga na hautakubali kuwekewa Rais.

"Huu ndiyo msimamo wangu, tutafanya vipi? Hiyo ni mikakati ya chama, huwezi kuwa na mkakati ukautangaza hadharani, wajue wakati huu hatutakubali," alitamba.

Maalim Seif pia aliulizwa na waandishi kuhusu shinikizo la baadhi ya vyama vya siasa kipindi hiki kudai nchi iwe na tume huru ya uchaguzi na akajibu kuwa serikali haiwezi kusema kutakuwa na uchaguzi wa huru na haki.

"Rais Magufuli anachopaswa kufanya, kwanza akutane na vyama vya upinzani na wajadili suala la tume huru, majadiliano yatakayokuwapo watafika mahali watasema hapa tumesikilizana, ikiwa vigezo hivi vitatumika, basi wataridhika," alisema.

Hata hivyo, Maalim Seif alisema hata yakiwapo mazingira ya aina gani, kama chama kimejipanga vizuri na kinawafikia wananchi, uwezekano wa kushinda upo.

"Siyo kwamba sisi tunapiga kelele tu, wala hatuwezi kusema tususie uchaguzi ili tumwachie nguruwe mhogo, mwaka huu hatususii uchaguzi, msimamo wetu ACT-Wazalendo, hatususi," alihitimisha.

## HABARI KITAIFA



Raia wa Cameroon, Johnson Table, akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuhukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 100 au kwenda jela miaka mitatu, baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na Dola za Marekani 84,300 bila maelezo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wagonjwa wanaume na wanawake walala wodi moja

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

UHABA wa wodi katika Kituo cha Afya Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, umesababisha wagonjwa wa kike na kiume kulala sehemu moja.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Mganga Mfawidhi wa kituo hicho cha afya, Eradius Kweyamba.

Aliyasema hayo kwenye halfa ya kupokea msaada wa magodoro 15 na vitanda 18 vikiwamo vya kujifungulia vyenye thamani ya Sh. milioni 11.2 kutoka kampuni ya Alliance One inayojihusisha na ununuzi wa zao la tumbaku katika wilaya hiyo.

Kweyamba alisema kituo hicho kinaupungufu na ufinyu wa wodi za kulaza wagonjwa hali inayosababisha wagonjwa wa kiume na kike pamoja na watoto kulazwa katika wodi moja.

Alisema kituo hicho cha afya kinapokea wagonjwa 30,000 kutoka katika kata za Ulowa, Uyogo, Bukomela na wilaya za mkoa wa jirani wa Tabora ikiwamo wilaya za Kaliua, Uyui na Urambo.

Alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo ufinyu wa maabara unaosababisha kukosekana kwa chumba cha damu salama, ukosefu wa mashine ya Ultrasound, jengo la upasuaji ambalo halikidhi viwango, upungufu wa matundu ya vyoo.

Akizungumza wakati akikabidhi msaada wa vifaa hivyo, Meneja wa Tumbaku wa Kampuni ya Alliance One Mkoa wa Kitumbaku Kahama, Marcean Mayunga, alisema kampuni ya Alliance One inaunga mkono juhudi za serikali za kuboresha huduma za afya katika halmashauri hizo na kwamba itaendelea kuboresha hudma za afya ya mama na mtoto pamoja na wagonjwa wengine wanaopatiwa huduma kituoni hapo.

"Ninaamini kila kitu tunachokifanya na kusaidia katika jamii ni kubadilisha maisha ya watu ili sote tuishi maisha bora hapa duniani," alisema Mayunga.

Alisema kutokana na changamoto zilizopo kituo hicho cha afya, ataziwasilisha kwa mkurugenzi wa kampuni hiyo ili waone namna ya kuzitatua.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Nicodemas Sengui alisema: "Ninawashukuru kwa msaada huu na ninawaomba msichoke kuendelea kutusaidia kituo hiki ambacho kinakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo kulaza wagonjwa wa jinsia zote katika wodi moja pamoja na watoto."

Alisema kituo hicho kina wodi mbili, moja ni ya wazazi nyingine ni wagonjwa mchanganyiko, kina watoa huduma wa afya 27, madaktari watatu.

# Raia Cameroon ahukumiwa kulipa faini ya mil. 100/-

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Cameroon Johnson Table (32), amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 100 au kwenda jela miaka mitatu baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na Dola za Marekani 84,300 bila maelezo.

Kadhalika mahakama hiyo imetaifishwa Dola za Marekani 84,300 alizokutwa nazo kuwa mali ya serikali baada ya mshtakiwa kukiri kosa la kukutwa na fedha hizo bila maelezo.

Hukumu hiyo ilisomwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Table alilipa faini hiyo na kuachiwa huru.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mkuu, Shadrack Kimaro, alimsomea mshtakiwa mashtaka yake na kukiri.

Kimaro aliomba mahakama pamoja na adhabu ya kulipa faini, fedha za kigeni alizokutwa nazo zitaifishwe kuwa mali ya serikali.

Wankyo, alidai kuwa Februari 27, mwaka huu, katika Uwanja Ndege wa Julius Nyerere, uwanja namba tatu, mshtakiwa akiwa safarini kutoka nchini alikutwa na Dola za Marekani 84,300 bila maelezo kwa Mamlaka ya Forodha ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Baada ya kusomewa mshtakiwa alikiri makosa na kusomewa maelezo ya awali dhidi ya mashtaka yanayomkabili.

Mshtakiwa ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Linde, Cameroon, aliingia nchini Februari 26, mwaka huu, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo Mamlaka ya Forodha, wakati anaingia nchini hakueleza kama anaingia na fedha zozote.

Februari 27, alikuwa akiondoka nchini kupitia ndege ya Rwanda na alikuwa na tiketi ya kielekitroniki pamoja na hati ya kusafiria.

Ndege hiyo ilikuwa ikiondoka saa 11.40 jioni kuelekea Kigali na baadaye Duoala, Cameroon.

Mshtakiwa alikuwa ameshika begi, akiwa uwanjani alianza utaratibu wa kuingia na akapita kwenye mashine ya kwanza ya ukaguzi, alipoenda kwenye mashine ya pili ili aingie kwenye chumba cha kusubiria abiria, kitu kisicho cha kawaida kiligundulika katika begi lake.

Inadaiwa alielekezwa aache mkoba wake kwenye mashine kwa mara ya pili na kitu kisicho cha kawaida kilibainika.

Ilidaiwa kuwa aliamriwa kutoa kila kitu kilichokuwa kwenye begi, fedha hazikuwa miongoni mwa vitu vilivyotolewa.

Begi lilipowekwa kwenye mashine ilibaika kuwa ndani zilifichwa fedha na lilipopekuliwa ilibainika Dola za Marekani 84,300.

Fedha zilizokamatwa ziliwekwa kwenye akaunti katika Benki ya NMB na namba zake zilinakiliwa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 04/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 08/03/2020 kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCTION& INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **INYONGA** kuelekea **KABANGA,** kupitia **MPANDA** Magari hayo yana namba za usajili:
**T550 BES/ T 474 BCJ**
**T389 BES/ T668 BCJ**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 16** |
| **Upana** | - | **mita 2.7** |
| **Kimo** | - | **mita 4.9** |

3. Njia itakayotumika: **INYONGA hadi KABANGA** kupitia **MPANDA** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115654902



**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**Invitation to bid: No. ITB/2020/SUP/002**

**ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENT(S) FOR THE SUPPLY OF DIESEL FUEL – BULK DELIVERY**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Tanzania, invites qualified suppliers to make a firm offer for the establishment of Frame Agreement(s) for the supply of Fuel (Diesel) Delivered in Bulk to the destinations mentioned below.

UNHCR may award Frame Agreement(s) with initial duration of 2 (two) years, potentially extendable for a further period of 1 (one) year, for supplying its operation in Tanzania. The successful bidders will be requested to maintain their quoted price model for the duration of the Frame Agreement(s).

**2. Eligibility:**

Fuel Companies, authorized resellers, wholesalers, or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be downloaded from link here
**https://drive.google.com/drive/folders/1TsJo5j3LqD-ZeHWG5dT80gr-80nFka6l**

**CRUCIAL DATES FOR THIS INVITATION TO BID**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Tuesday 17th March 2020 at 23.59 hours EAT |
| Suppliers' conference meeting | Wednesday 18th March 2020 at 11.00hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Tuesday 14th April 2020 at 16.00 hours EAT |

***UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to access the tenders.***

215649302

# Majaliwa awapa angalizo wenyeviti vijiji wauza ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameonya tabia ya baadhi ya wenyeviti wa vijiji wanaofanya biashara ya ardhi waache na badala yake amewataka wajihusishe katika kutekeleza majukumu yao ya msingi.

Alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa Shule ya Msingi Bokwa wilayani Kilindi akiwa kwenye ziara yake ya kikazi mkoani Tanga.

Waziri Mkuu alisema tabia ya baadhi ya wenyeviti wa vijiji kujihusisha na biashara ya uuzaji wa ardhi inachangia kuwapo kwa migogoro, hivyo aliwataka wasijihusishe na masuala hayo.

"Wanaouza ardhi za vijiji bila ya kuwa na vibali vya halmashauri wachukuliwe hatua kwa sababu ndio wanaosababisha migogoro ya ardhi. Viongozi acheni tabia ya kuwaingiza wananchi kwenye migogoro."

Pia, Waziri Mkuu alionya tabia ya wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima. "Haikubaliki na haiingii akilini katika hali ya kawaida mtu amelima shamba lake la chakula halafu mwingine anaenda kuingiza mifugo haikubaliki."

Waziri Mkuu aliongeza: "Kama unadhani mahindi ndio chakula bora cha ng'ombe wako lima ulishe mifugo. Hakuna Mtanzania aliyeko juu ya sheria kama kuna mtu ameua kwa kulinda ng'ombe wake, Mkuu wa Wilaya fanya uchunguzi wa jambo hilo na hatua zichukuliwe."

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliodai kuna mkulima ameuawa na mfugaji kutokana na mgogoro uliotokea wakati mfugaji alipoingiza mifugo kwenye shamba la mkulima.

Akizungumzia kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya wilaya ya Kilindi (Tanga) na Kiteto (Manyara), alisema suala hilo iachiwe Serikali kwani tayari imeshaanza kulishughulikia.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesema Wilaya ya Kilindi itajengewa hospitali ya wilaya ili kuwapunguzia wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Pia, aliwataka wananchi waendelee kuiamini Serikali yao na kwamba changamoto mbalimbali zinazowakabili zikiwemo za upatikanaji wa huduma za maji, umeme na miundombinu ya barabara zitafanyiwa kazi.

Kadhalika, Waziri Mkuu alizindua mradi wa maji wa Bokwa na amesema kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ina mikakati mizuri inayolenga kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo na Wilaya ya Kilindi.

Awali, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa kituo cha afya cha Mswelo kilichopo kwenye Kata ya Kwediboma, ambapo amesema awali Serikali ilitoa Sh. milioni 300 kwa ajili ya ujenzi huo na itaongeza Sh. milioni 200 ili kituo hicho kikamilike.

# Kunradhi Xavier Kundi

KATIKA toleo letu Na. 0580099 la Desemba 12, mwaka jana, tulichapisha habari kwenye ukurasa huu ikiwa na kichwa kilichosomeka 'Kigogo TRC ahukumiwa kulipa milioni 100/-'.

Kimsingi habari hiyo ilikuwa inahusu hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam kumhukumu mtumishi huyo wa zamani wa Shirika la Reli (TRC) kulipa fidia ya Sh. 108,400, baada ya kupatikana na hatia ya wizi akiwa mtumishi wa shirika hilo, lakini tukaandika kimakosa kiwango cha fidia kwamba ni Sh. milioni 108.4.

Pia, katika kichwa cha habari tulichoandika siku hiyo, tulimtaja kimakosa Kundi kwamba ni 'kigogo wa TRC' ilhali alikuwa mtumishi wa kawaida ndani ya shirika hilo.

Tunamwomba radhi Kundi na wasomaji wetu kwa usumbufu wowote uliojitokeza kutokana na habari yetu hiyo.


The Guardian Limited

## JOB VACANCY

The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:

### CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM

**Job Purpose:**
To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:
- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;vacancy@guardian.co.tz by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302


# Kesi mfanyabiashara J4 yaanza kusikilizwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KESI ya mauaji namba 131 ya mwaka 2017 inayomkabili mfanyabiashara na mmiliki wa mabasi, Jumanne Wang'anyi, maarufu kama J4, mkazi wa Nyakato jijini Mwanza, imeanza kusikilizwa na kutolewa ushahidi katika Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza.

Kesi hiyo ilianza kusikiliza juzi mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Sam Rumanyika, Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili Robert Kidando na Upande wa Utetezi unaongozwa na Wakili Anthony Nasmir.

Mbele ya Jaji Rumanyika, shahidi wa kwanza, Donatha Gabriel, ambaye ni mke wa marehemu Ally Abeid, na shahidi wa pili, Aziza Sekarwanda, ambaye ni dada wa marehemu Cloud Sekarwanda, walidai mahakamani kuwa mnamo Julai 13, 2015 ambayo ni siku ya tukio hilo la mauaji, waliagwa na Abeid na Sekarwanda (wote marehemu) kuwa wanakwenda kuonana na bosi wao ambaye ni mfanyabiashara huyo. Inspekta Benidict Manyanda ambaye ni shahidi wa tatu katika kesi hiyo, alidai mahakamani kuwa siku ya tukio, alifika eneo la tukio na kukuta miili ya watu wawili ikiwa chini na baadaye kuipelekea hospitali kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Akitoa ushahidi wa tukio hilo, shahidi wa nne, Inspekta wa Polisi Masaga Francis kutoka Kitengo cha Uhalifu kwa Njia ya Mtandao, alidai mahakamani hapo kuwapo kwa mawasiliano ya kimtandao baina ya marehemu Abeid na mshtakiwa J4 kuanzia Mei 2015 hadi Julai mwaka huo na hata siku ya siku hiyo ya tukio.

Mfanyabiashara huyo anadaiwa kuwa Julai 13, 2015, aliwaua kwa kuwapiga risasi wafanyabiashara wanzake wawili; Ally Abeid na Cloud Sekarwanda, eneo la Nyakato Boma lililoko sehemu ya kuhifadhi magari ya kampuni ya mshtakiwa huyo.

Jaji Sam Rumanyika aliahirisha kesi hiyo hadi kesho itakapotajwa tena huku mtuhumiwa akirudishwa mahabusi kwenye Gereza Kuu la Butimba jijini.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, akifungua bomba la maji katika eneo la Soko wilayani Kisarawe jana, ikiwa ni ishara ya upatikanaji wa huduma ya majisafi baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa), uliogharimu Sh. bilioni 10.6. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kabudi kuongoza wajasiriamali Comoro

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki , Prof. Palamagamba Kabudi ,ataongoza msafara wa wanawake wajasiriamali nchini (TASWE) kwenda Comoro kushiriki kwenye maonyesho ya biashara.

Lengo ni kuona fursa za kibiashara zilizopo visiwani humo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa TASWE, Anna Matinde, alisema TASWE kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Comoro wameandaa maonyesho hayo yakilenga kunadi na kuuza bidhaa za wajasiriamali ambazo zimekuwa na uhitaji mkubwa katika nchi ya Comoro.

"Kumekuwa na wajasiriamali wengi nchini ambao wamekuwa wakisindika na kutengeneza bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na hata uvuvi. Changamoto kubwa kwa wajasiriamali hao ni soko la ndani ambalo ushindani wake umekuwa mkubwa, TASWE tumeandaa maonesho haya ya bidhaa nchini Comoro kwa sababu uhitaji wa bidhaa hizo ni mkubwa," alisema.

Alisema maonyesho hayo ambayo yatajuimusha wajasiriamali 60 kutoka Tanzania na 150 kutoka Comoro yatafanyika kuanzia Aprili 17 hadi 24, 2020.

Aidha B Matinde alisema TASWE itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali za ujenzi wa uchumi wa kati kwa kuwatafutia fursa akina mama wajasiriamali ndani na nje ya nchi.

"Serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara na wajasiriamali jambo ambalo limeongeza uwepo wa bidhaa nyingi katika soko la ndani, hivyo tunaunga jitihada za serikali kwa kuhakikisha kila fursa inayopatikana inatumika ili kuinua kipato cha Watanzania," alieleza Matinde.

Matinde alitoa wito kwa wanawake wajasiriamali kujitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zinazojitokeza kwani zitachochea kuwainua wanawake kiuchumi na nchi kwa uchumi.

Kwa upande wake, Careen Meela, mjasiriamali wa bidhaa za Kilimo, alisema ziara hiyo itamsaidia kwa kiasi kikubwa kupata soko la uhakika wa bidhaa zake kwa kuwa amekuwa na uzoefu mkubwa wa kufanya biashara nchini Komoro.

Naye Consolata Rugasila, mfanyabiashara wa madini, aliwataka wanawake waache kulalamika na badala yake wajitokeze mstari wa mbele katika kufanya shughuli za maendeleo ikiwamo ujasiriamali.

# Viongozi dini waombwa kusaidia vita ya corona

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imesema, hadi kufikia jana, hakuna taarifa ya kifo cha ugonjwa unaotokana na virusi vya corona wala mtu mwenye dalili za ugonjwa huo nchini, huku ikiwaomba viongozi wa dini kusaidia katika mapambano hayo.

Hata hivyo, Watanzania wametakiwa kuendelea kuchukua tahadhari kuhakikisha virusi hivyo havingii nchini na kama ukiingia nchini, usisambae.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto, Ummy Mwalimu, wakati akifungua mkutano wa viongozi wa dini.

Mkutano huo ulihusu njia za kukabiliana na ugonjwa wa ebola na virusi vya corona Tanzania, ambapo aliwahimiza viongozi wa dini kusaidiana na serikali katika vita dhidi ya virusi vya corona.

"Hadi sasa nchi iko salama, hakuna kifo wala mgonjwa mwenye virusi vya corona, mimi ninaamini tuko salama kwa dua na sala zenu viongozi wa dini," alisema Ummy.

Aliwataka viongozi wa dini kuendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha kwamba hata ukiingia nchini usiwe na madhara, kwa vile wananchi watakuwa wameelewa jinsi ya kijikinga.

"Takwimu za leo (jana) za WHO (Shirika la Afya Duniani), zinaonyesha kuwa watu 90,870 wameambukizwa virusi hivyo na pia 3,112 wamefariki dunia, na ugonjwa huu sasa upo nchi 72," alisema.

Aidha, alisema katika Afrika kuna nchi nne zilizoripotiwa kukumbwa na ugonjwa huo, ambao ni Algeria, Misri, Senegal na Nigeria.

Aliwahakikishia Watanzania kuwa serikali haijalala na inaendelea na jitihada kukabiliana na tishio la ugonjwa huo kwa kila njia.

Alifafanua kuwa imeweka wataalamu wa afya na vifaa maeneo yote yakiwamo ya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege ili kupima abiria wanaoingia nchini.

"Vilevile, niwaombe wale watu wanaowatia wengine hofu waache kufanya hivyo, badala yake jamii ipate elimu sahihi ya kujikinga na corona," alisema.

Kwa mujibu wa Ummy, elimu hiyo ni watu kutopeana mikono, kutokumbatiana na pia kunawa kama njia mojawapo ya kusaidia kuwa salama.

Waziri alisema, viongozi wa dini wana ushawishi mkubwa katika jamii na waumini wao kwa ujumla, hivyo anaamini wana mchango wa kuhamasisha waumini kuzingatia kile ambacho kinaelekezwa katika kukabiliana na ugonjwa na hata kuondoa taarifa zisizo sahihi ambazo baadhi ya watu wanaeneza na kuwatia wengine hofu.

kwa upande wake Mwenyekiti wa Ushirika wa Dini na Taasisi za Kidini (Tanzania Interfaith Partnership), Mchungaji Canon Moses Matonya, aliishukuru serikali kwa ushirikiano wanaoupata.

"Kwa ujumla tunafanya kazi vizuri kwa kushirikiana na serikali na sasa tumeomba kuelimishwa kuhusu magonjwa hayo ili nasi tuifikishe kwa waumini makanisani na misikitini, " alisema Matonya.

Naye Sheikh Twahir Amran kutoka Misenyi mkoani Kagera, aliomba serikali itenge fedha kwa viongozi wa dini ili waweze kufanya kazi kuelimisha waumini kwa ufanisi.

Sheikh Amran alisema muda wa ibada hautoshi kutoa elimu, hivyo wanahitaji kutenga muda wa ziada tena maeneo tofauti na kutoa elimu hiyo.


**TANZANIA WILDLIFE MANAGEMENT AUTHORITY**

**NOTICE TO THE GENERAL PUBLIC**

**POSTPONEMENT OF ELECTRONIC AUCTIONING OF VACANT HUNTING BLOCKS**

Tanzania Wildlife Management Authority (TAWA) wishes to inform the general public that, Hon. Dr. Hamisi A. Kigwangalla (MP), Minister for Natural Resources and Tourism of the United Republic of Tanzania has postponed the electronic auctioning of vacant hunting blocks which was scheduled on 5th March 2020 till further notice.

The decision is made due to complaints from some stakeholders.

Thus, this is to allow consolidation of the said complaints before conducting the third phase of the said e- auctioning. The new auction date will be communicated to you in due time. We sincerely regret for inconvenience caused.

**Issued by:**

**Conservation Commissioner**
**Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA Morogoro Road-Kingolwira Area**
**TAFORI Building**
**PO Box 2658**
**Morogoro - Tanzania**

**Tel: +255 (0) 23-293424**
**E-mail: cc@tawa.go.tz**

215655302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rais Magufuli, upinzani kukutana mwanzo mpya

**RAIS** John Magufuli juzi alikutana na kufanya mazungumzo na wanasiasa watatu; Maalim Seif Sharif Hamad, Prof. Ibrahimu Lipumba na James Mbatia, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Baada ya mazungumzo hayo, Maalim Seif Sharif Hamad ambaye aliwahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alisema yeye na Rais Magufuli walizungumzia masuala ya kudumisha amani, usalama na upendo kwa watu wote.

Alisema amefurahishwa na dhamira ya Rais Magufuli kukutana na viongozi mbalimbali na kujadiliana mambo yenye maslahi kwa nchi.

Prof. Lipumba ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), alimpongeza Rais Magufuli kwa ahadi yake kuwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu utakuwa huru na wa haki.

Mtaalamu huyo wa uchumi pia alipongeza juhudi zinazofanywa na serikali kupambana na rushwa, kudhibiti matumizi mabaya ya serikali, kulinda na kutumia vizuri rasilimali za taifa, kuboresha elimu na kuimarisha uchumi.

Alitoa wito kwa Watanzania wote kuweka uzalendo mbele na kudumisha amani na utawala bora.

Naye Mbatia, mbali na kufurahishwa na dhamira ya Rais Magufuli juu ya Uchaguzi Mkuu kuwa huru na wa haki, aliwataka wanasiasa waache kukamiana na kuchochea mambo hasi dhidi ya taifa, badala yake waungane kuendeleza mambo mazuri yanayofanywa na serikali ikiwamo kuboresha elimu, upatikanaji wa nishati na mengine yenye maslahi mapana kwa wananchi.

Mbatia alitoa wito kwa wanasiasa na Watanzania wote kwa ujumla kuweka mbele maslahi ya taifa badala ya kukumbatia mambo yenye maslahi binafsi.

Hii ni mara ya kwanza kwa Rais Magufuli kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa upinzani tangu aingine madarakani mwaka 2015.

Tunaipongeza hatua ya Rais ya kuanza kukutana na vyama vya siasa kwa ajili ya kusikiliza maoni yao pamoja na kushauriana kuhusiana na mambo mbalimbali ya nchi yetu yenye maslahi mapana ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Jambo la kutia moyo ni kuwa mazungumza hayo yamefanyika katika kipindi ambacho taifa letu linajiandaa kufanya uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu, hivyo ni kiashiria kwamba uchaguzi huo utafanyika katika mazingira rafiki, ambayo pande zote zinasikilizana na kushauriana.

Kauli zilizotolewa na viongozi hao watatu wa upinzani zinadhihirisha kuwa wanatanguliza mbele umoja wa kitaifa na maslahi mapana ya taifa letu.


Jambo walilolisisitiza la kuwapo kwa uchaguzi huru na haki lilishazungumziwa na Rais Magufuli alipokutana na mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa mwaka huu, hivyo kudhihirisha kuwa serikali imedhamiria kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika katika mazingira rafiki.

Tunashauri kwamba milango aliyoifungua Rais Magufuli iendelee kuwa wazi kwa viongozi wa vyama vingine vya siasa nchini kwa lengo la kuendeleza majadiliano na mashauriano yenye lengo la kuhakikisha kuwa uchaguzi wa mwaka huu unakuwa wa amani na salama.

Huu ni wakati kwa vyama vya siasa ambavyo vitapata fursa ya kukutana na Rais kwenda na ajenda ambazo zina lengo la kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

Vinginevyo, tunasema kuwa hatia ya Rais ni mwanzo mpya, hivyo fursa ya kukutana naye itumiwe vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamani, tukwepe corona kwa staili toka kwa viongozi wetu

Na Sabato Kasika

**DUNIA** sasa inakabiliwa na wasiwasi kutokana na virusi vya corona, ambavyo vimeanzia nchini China na sasa vinadaiwa kusambaa kwenye baadhi ya nchi, huku ikielezwa kuwa vimesababisha vifo zaidi ya 2,000.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema dunia imeingia hali ya shaka ya vita dhidi ya virusi hivyo, kwamba wakati kasi ya maambukizi mapya imeshuka nchini China, lakini kwingine inaongezeka kwa kasi.

Wakati juhudi za kukabiliana na virusi hivyo zikiendelea, serikali ya Tanzania imeanza kuchukua hatua za kuhakikisha wananchi wake wanakuwa salama.

Miongoni mwake ni ile iliyotangazwa wiki iliyopita na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akiwataka Watanzania kuacha tabia ya kukumbatiana na kupeana mikono.

Anasema, japo virusi vya corona havijaingia nchini, lakini Watanzania wanatakiwa kuepuka kusalimiana kwa mtindo huo katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa huo unaoendelea kutikisa dunia.

Ni hatua inayoangukia katika 'kinga ni bora kuliko tiba.' Hivyo, kila mmoja hana budi kuzingatia maelekezo hayo na kuyafanyia kazi, kuliko kuzembea na kujikuta katika matatizo.

Wizara inasema suala la kuacha kusalimiana kwa kupeana mikono au kukumbatiana linaweza kuwa gumu, lakini pamoja na ugumu huo, jambo la msingi ni kuacha mazoea ili kujihakikishia usalama zaidi.

Kila mmoja anatakiwa kuepuka kugusana na mtu mwenye dalili za magonjwa ya njia ya hewa, hususani mwenye historia ya kusafiri katika maeneo au nchi zilizoathirika na ugonjwa huo.

Viongozi wakuu wa nchi wameitikia maelekezo hayo na wameanza kuyafanyia kazi. Kwa mfano huo, Watanzania kwa ujumla wao nao hawana budi kuiga njia za viongozi wao.

Kwa kutii maelekezo hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa mkoani Tanga alisalimiana na viongozi wa mkoa kwa mbali, bila ya kugusana kama ambavyo wizara husika imeagiza.

Rais John Magufuli, pia katika njia hiyo, alionekana akisalimiana na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa kwa kugonganisha viatu tu, bila kushikana mikono lengo ni kutimiza maelekezo ya usalama wa afya.

Sasa ni vyema hiyo ikawa njia yetu wengine, tukiiga mfano huo ili kuiweka nchi salama dhidi ya virusi vya corona ambavyo vimeshapoteza maisha ya wenzetu wengi duniani.

Ni wakati wa kutofanya mambo kwa mazoea, badala yake kuzingatia ambacho kinaelekezwa kwa ajili ya usalama, kuliko kusubiri majanga yatokee, kushtuka.

Jamii inapaswa ichukue malekezo hayo kwa umakini bila ya kuhoji utaalamu ambao umeshafanyiwa kazi. Kwani, tangu serikali itangaze hatua hizo zenye lengo la kukabiliana na virusi, wapo baadhi ya watu wameanza kusema wanavyojua wao.

"Kama Mungu amekupangia kufa kwa virusi vya corona utakufa tu, hata bila kupeana mikono au kukumbatiana, na wengine," ni sehemu ya matamshi, wakiona ni vigumu kuacha salamu hizo.

Binafsi kauli kama hizo ninaziita kwa jina la 'uzembe' ambao hautakiwi kupewa nafasi, badala yake wale wanaojitambua wazingatie kile ambacho kimeelekezwa na serikali kwa ajili ya usalama wetu sote.

Kama hawajui, basi wakumbushwe kutambua 'kinga ni bora kuliko tiba.' Wajifunze kupitia msemo wa 'kubadili gia angani' kuliko kung'ang'ania mazoea ambayo mwisho wake ni mbaya.

Ushauri huu wa kujizuia kupeana mikono na kukumbatiana usipite kienyeji, bali uzae matunda na wale wenye mawazo kwamba kuachana na matindo huo haiwezekani, wanafaa kurejeshwa darasani, maana elimu haina mwisho.

Umuhimu wa kupeana mikono au kukumbatiana wakati wa kusalimiana ni upi, kama siyo mazoea na utamaduni? Pia ni vyema kukumbuka kwamba mazoea yana taabu.

Siyo vizuri kuishi kwa mazoea, badala yake ni wakati wa kuishi kulingana na mazingira na jinsi dunia inavyokwenda, kama ambavyo sasa inapambana na virusi vya corona

Kila mmoja kwa njia moja ama nyingine ana nafasi ya kushiriki katika vita dhidi ya virusi hivyo, madaktari wanafanya sehemu yao na wananchi kwa upande wao, wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu hao wa afya.

# Ikungi yazawadia walimu, wanafunzi

**Na Elisante John,** IKUNGI

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida, imetoa zawadi za vyeti na fedha taslimu kwa shule zilizofanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa kwa mwaka jana.

Akizungumza kwenye hafla ya kugawa fedha na zawadi iliyofanyika katika sekondari ya Ikungi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi, alisema jambo zuri linapofanyika halinabudi kuungwa mkono na wengi ili kujenga morali kwa wanaolifanya.

Alizitaja shule kumi za msingi zilizozawadiwa ni Msule, Utaho, Musambu, Kituntu, Puma, Nkuninkana, Mankumbi, Dung'unyi, Matyuku na Lainihungu, huku walimu wakiwa ni Yasini Hamisi, Petro Mimbi, Elisha Charles, Adinan Musa, Piniel Gidiba na Richard Wedy.

"Utaratibu huu utatusaidia kuinua taaluma kwenye shule zetu, hivyo kila mwanafunzi na walimu wao wataongeza juhudi zaidi ili kila mmoja aweze kushinda zawadi hizi za fedha zinazoanzia na Sh. 20,000 hadi Sh.70,000," alifafanua Kijazi.

Kwa upande wa sekondari, Ofisa Elimu Taaluma wa Halmashauri hiyo, Andrew Marwa, alisema kwa miaka miwili mfululizo ufaulu wa kidato cha nne umeongezeka kutoka asilimia 83.27 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 93.43 mwaka jana.

Kwa upande wa kidato cha pili, alisema kuwa mwaka jana 2018 ufaulu ulikuwa asilimia 94.2 kitaifa ikiwa ni halmashauri ya 71 kati ya 184, wakati mwaka jana ufaulu ulishuka kidogo hadi kufikia asilimia 93.35, huku kitaifa ikishika nafasi ya 82 kati ya 184.

Akikabidhi viti na meza 500 kwa shule za sekondari zenye upungufu na mengine 990 yaliyokarabatiwa, mgeni rasmi Katibu Tawala wa Wilaya ya Ikungi, Winfrida Funto, aliwataka watumiaji kuvitunza ili viwe endelevu.

Kiongozi huyo, alimwakilisha Mkuu wa Wilaya, Edward Mpogolo.

Vitendea kazi vingine vilivyokabidhiwa kwenye hafla hiyo ni vifaa vya maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi na taulo za kike zikiwa kwenye makasha 3,550, kwa ajili ya wasichana wanaosoma shule za sekondari wilayani humo.

Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imetumia jumla ya Sh. milioni 35.5 kutengeneza seti za viti na meza 830, zikiwamo Sh. milioni 11.5 za mapato ya ndani, huku Shirika la Taifa la Hifadhi za Taifa (Tanapa) likitoa Sh. milioni 24.

Ikungi ina jumla ya shule za msingi 111 na sekondari 36, wakati kwa mwaka jana shule 108 za msingi zilifanya mtihani wa darasa la saba na shule 36 za sekondari zilifanya mtihani wa taifa kidato cha nne na upimaji wa kidato cha pili.

# Wenye bajaji wataka punguzo kodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAMILIKI wa bajaji za mizigo na abiria wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa Maalumu wa kikodi Kahama, kuwapunguzia kodi kutoka Sh. 250,000 wanazolipa sasa hadi Sh. 100,000.

Walisema mwaka jana walikuwa wakilipa kodi ya Sh. 150,000 na kila mmoja alilipa kwa wakati, na kwamba na mwaka huu kodi imeongezeka, hadi Sh. 250,000 sawa na ongezeko la Sh. 100,000.

Ombi hilo lilitolewa na wamiliki wa vyombo hivyo katika mkutano wa hadhara ulihudhuriwa na maofisa wa TRA Kahama, na kusema kuwa ongezeko la kodi limesababisha baadhi yao kuamua kuuza vyombo hivyo.

Richard Thomas, katibu msaidizi wa bodaboda na bajaji mkoani Shinyanga, alisema wamiliki wa bajaji za mizigo na abiria wanatishia kuuza bajaji zao, kutokana na ongezeko kubwa la kodi.

"Tumekuwa tukipokea malalamiko mengi ya ongezekao la kodi...nilifanya utafiti wa kina ni nani mpaka sasa ameshalipa kodi baada ya ongezeko hili, na nilibaini mtu mmoja ambae nae alikuwa amelipa nusu ya kodi, na kuhamishia bajaji yake jijini Mwanza," alisema.

Aidha, alisema Wilaya ya Kahama ina zaidi ya bajaji 1,400, huku bajaji za mizigo zikiwa 800 na abiria zikiwa 600, kuwa endapo TRA itapunguza kodi na kufikia Sh. 100,000, wataweza kulipa kodi kwa wakati na kuachana na kuuza vyombo hivyo.

Thomasi alisema, endapo kodi hiyo itapunguzwa, atahakikisha kila mmiliki analipa kodi hiyo kwa wakati, na kuwa na kuwa atakatekaidi, atawajibishwa kwa sheria za chama.

Nae Juma Shagile, alisema wamiliki wa bajaji katika Jiji la Dar es Salaam na Mwanza wanalipa kodi ya Sh. 100,000.

Kaimu Meneja wa TRA Kahama, Willison Makalanga, alisema wamiliki wa bajaji jijini Dar es Salaam na Mwanza wanatoa kiasi hicho cha kodi kutokana na kuwa na ushindani wa kibiashara na wamiliki wa daladala.

Hata hivyo, Makalanga alisema ombi la kulipa Sh. 100,000 alelichukua na atalifanyia kazi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, Justice Kijazi, akizungumza na walimu na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kabla ya kutoa zawadi kwa shule 10 za msingi zilizofanya vizuri mwaka 2019, na kugawa vifaa vya maabara na madawati kwa shule za sekondari yaliyotolewa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), jana. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Viongozi dini wanolewa uhalifu wa mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Amani Mkoa wa Morogoro imetoa wito kwa taasisi nchini kuiga mfano wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika kuelimisha viongozi wa dini kuhusu kujikinga na uhalifu wa mawasiliano kwani wao wana wafuasi wengi na ushawishi mkubwa katika jamii.

Kauli hiyo waliitoa jana wakati wa semina ya Kamati ya Amani ya Mkoa Morogoro inayotolewa na TCRA kwa kutoa elimu juu ya utumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kujikinga na uhalifu unapotumia huduma hizo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Juma Ng'odavi, alisema kuna umuhimu kupata semina ya huduma za mawasiliano kwa kuwa wao wanazunguka jamii yote ya mkoa huo, ambao wengi wao wanatumia huduma za mawasiliano.

Alisema kazi yao kubwa kama mabalozi baada ya semina hiyo ni kutoa elimu katika nyumba za ibada na kwa viongozi ambao hawajafika katika semina hiyo ili waweze kupokea elimu ya kujikinga na uhalifu wakati unapotumia huduma za mawasiliano.

Naye Katibu wa Makanisa Mkoa wa Morogoro na Mjumbe wa Kamati ya Maridhiano Mkoa huo, Mchungaji Canon Regnald Mdugi, alisema elimu walioipata TCRA wataipeleka kwa waumini kwa kuhakikisha wanaelewa kujikinga na uhalifu wakati kutumia mitandao ya mawasiliano.

Naye Mwakilishi wa Mkuu wa Kanda ya Mashariki wa TCRA, Christopher John, alisema kampeni ya kuelimisha jinsi ya kujikinga na uhalifu wakati wa kutumia huduma za mawasiliano, ni sehemu ya kampeni ya 'Sirubiniki Mjanja Haingizwi Chaka' inalenga kuelimisha umma kujikinga na uhalifu wa mitandao.

Naye Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema wanafikia makundi yote katika kampeni hiyo na kwamba wakati umefikia wa watu kutumia mawasiliano kwa kulinda usalama wa nchi pamoja na wanaotumia mawasiliano bila kufuata sheria na taratibu, mkono wa sheria utawakuta.



Wachuuzi wakiwa wamepanga bidhaa zao pembeni ya barabara katika eneo la Ilala Boma, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu kwa waenda kwa miguu. **PICHA: MIRAJI**

# Chadema yajitosa sakata la Lema

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimetangaza kuchukua hatua za kisheria ili kuhakikisha mjumbe wa Kamati Kuu wao, Godbless Lema, anapata haki ya kuachiwa huru kwa dhamana au kufikishwa mahakamani.

Kwa mujibu wa taarifa ya chama hicho iliyotolewa jana, hatua hizo zinachukuliwa baada ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida kuendelea kumshikilia Lema ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini.

Jumatatu ya wiki hii, Lema alisafirishwa kutoka Arusha hadi Singida na jeshi hilo na juzi lilimfanyia mahojiano.

"Katika hali ya kushangaza Polisi mkoani Singida kupitia Mkuu wa Upelelezi Mkoa (RCO), tangu kumalizika mahojiano hayo wameshindwa kumwachia kwa dhamana au kumfikisha mahakamani kama sheria zinavyoelekeza, badala yake wamedai wanasubiri maelekezo kutoka juu," ilieleza taarifa hiyo.

Katika taarifa hiyo, Chadema imelalamikia mwenendo huo wa Jeshi la Polisi kuwatendea watuhumiwa hasa viongozi, wanachama, wafuasi na wapenzi wa chama hicho kama wahalifu, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# Jalada kesi ya Magoti bado mikononi mwa polisi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeambiwa na Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Ofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti na mwenzake kwamba hauwezi kueleza upelelezi umefikia hatua gani kwa sababu jalada bado liko mikononi mwa polisi.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega pamoja na Jamhuri kuelezea hatua ya upelelezi ulipofikia.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba haiwezi kielezea hatua ya upelelezi ulipofikia kwa sababu jalada liko mikononi mwa polisi wanaendelea na upelelezi wake.

Alidai kuwa upepelezi utakapokamilika Jamhuri utaifahamisha mahakama.

Wakili wa utetezi Fulgence Masawe, aliiomba Mahakama iendelee kusisitiza Jamhuri kukamilisha upelelezi wa kesi hiyo.

Alidai kuwa shida ya utetezi ni, haki na ili haki itendeke ni lazima ionekane, maombi ya utetezi ni Jamhuri watie msukumo kwa polisi kukamilisha upepelezi, kesi haina dhamana washtakiwa wanasota rumande.

Hakimu Mtega alisema, Jamhuri wawasiliane na polisi wakamilishe upepelezi.

Alisema kesi hiyo itatajwa Machi 18, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Tito mshtakiwa mwingine ni, Mtaalamu wa Tehama, Theodory Gyan (36) wote kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kumiliki programu ya kompyuta iliyotengezwa mahususi kufanya kosa la uhalifu na kutakatisha Sh. milioni 17.3.

Upande wa Jamhuri uliowasomea mashtaka washtakiwa uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Joseph Pande na Wankyo Simon.

Katika kesi ya msingi, Wankyo alidai kuwa washtakiwa wote, katika tarehe kati ya Februari Mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya Jiji la Dar es Salaam na mahali tofauti nchini Tanzania kwa pamoja na watu ambao hawapo mahakamani kwa makusudi walishiriki kutenda makosa ya kiuhalifu ya kumiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kufanya kosa la jinai na kuwawezesha kujipatia Sh. 17,354,535.

Nchimbi alidai katika tarehe tofauti kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya jiji na Mkoa wa Dar es Salaam kwa pamoja washtakiwa hao na wengine ambao hawapo mahakamani walimiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kutenda makosa.

Mkude alidai katika shtaka la tatu, Inadaiwa kuwa kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019, jijini Dar es Salaam washtakiwa hao kwa pamoja walitakatisha na kujipatia Sh. 17,353,535 wakati wakijua mapato hayo yametokana na zao la kosa la kushiriki genge la uhalifu.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi mpaka ipate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mshataka nchini (DPP) au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

# Watoto mazingira magumu kurudishwa kwa wazazi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MANISPAA ya Kigoma Ujiji imeanza kuwakamata watoto wanaoishi mitaani kuongea nao na kufanya utaratibu wa kuwawezesha kukutana na familia zao.

Akizungumzia kazi hiyo iliyoanza Ijumaa iliyopita, Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Kigoma Ujiji, Agness Punjila, alisema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwamo Jeshi la Polisi wamekamata watoto 39 na kuwahoji ili kubaini chanzo cha kuondoka nyumbani.

Alisema kazi hiyo ni ngumu kwa kuwa watoto hao wanapobaini wanatafutwa hujificha au kukimbia, hivyo ili kufanikisha wanawavizia usiku wakiwa wamelala.

Pia, Punjila alisema watoto hao wanaishi katika mazingira hatarishi kutokana na kutumiwa kutekeleza vitendo vya uhalifu vya kupora na kujeruhi watu pamoja na kulala sehemu zisizo salama.

"Tumefanya mahojiano na baadhi ya watoto wamekubali kurudi nyumbani na wengine wamekataa hivyo watapelekwa katika vituo vya kulelea watoto kwa ajili ya tiba ya kisaikolojia na baadaye kuwakutanisha na ndugu zao," alisema.

Mwenyekiti wa kamati iliyoundwa ya kunusuru watoto wanaoishi mtaani na Mratibu wa Shirika la Msalaba Mwekunduku Kigoma, Harid Suleiman, alisema asilimia kubwa ya watoto waliowakamata wana wazazi, lakini kutokana na changamoto za kimalezi walikimbia nyumbani.

Suleimani aliwataka wahisani mbalimbali wanaotoa misaada kwa watoto hao mitaani kuacha na kutoa katika vituo vya kulelea watoto kwa kuwa uwapo wa wahisani hao unachangia watoto kuvutiwa na maisha hayo na kusababisha watoroke katika familia zao.

"Mimi nashauri zitungwe sheria za kuzuia watu kusaidia watoto hawa mtaani ili wakose fedha za kuendesha maisha na warudi nyumbani," alisema.

Mmoja wa watoto hao amepongeza hatua hiyo ya kukusanywa na kuomba kwa walioamua kurudi nyumbani warudishwe na wanaotaka kupelekwa katika vituo vya kulelea watoto wapelekwe.

# Ufugaji nyuki kuokoa uharibifu mazingira

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANANCHI wameshauriwa kufuga nyuki ili kutunza mazingira na kujiongezea kipato.

Ushauri huo umetolewa juzi mjini Kibaha, na Mjumbe wa Kamati ya Mazingira ya Jumuiya ya Wazazi, Kibaha Mjini, Ibrahim Mkwiru, alipokuwa akiongea na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa ufugaji nyuki.

Mkwiru alisema, ufugaji wa nyuki unaweza kusaidia kuanzia ngazi ya familia katika mapambano ya umaskini, na endapo uhamasishaji utafanyika maeneo mengi ni moja ya chanzo cha ukuaji wa uchumi kwa taifa.

Alisema, katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, vipo baadhi ya vikundi vimenufaika na mafunzo ya kufuga nyuki, lengo kuviwezesha kujiajiri na kutumia ufugaji huo kama shughuli yao ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

"Tunaunga juhudi za mapambano ya umaskini, tumekuwa tukiwashauri wananchi kutunza mazingira katika maeneo yao, lakini katika hili kuwahamasisha kufuga nyuki kama sehemu ya chanzo chao cha mapato," alisema Mkwiru.

Alisema, wananchi walionufaika na mafunzo ya ufugaji nyuki wamepatiwa mizinga kwa ajili ya kuanza kufuga.

"Tayari nimetoa mizinga 40 ya kufugia nyuki kwa vikundi vilivyopo ndani ya Jumuiya ya Wazazi wa CCM, wapo watu binafsi ambao pia wamepata na tayari wameanza ufugaji nitaendelea kusaidia kadri iwezekanavyo kulingana na mahitaji" alisema Mkwiru.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Kibaha Mjini, Edwin Shunda, alimshukuru Mkwiru kwa kufanikisha kupatikana kwa mizinga hiyo na mafunzo ya ufugaji ambayo yamefanyika kutekeleza agizo la jumuiya hiyo ngazi ya Taifa.

Mmoja wa wanufaika wa mizinga kwenye kikundi cha Mwambisi Kata ya Kongowe, Cleophamary Edwin, alisema, ufugaji wa nyuki ni kati ya mazao yanayosaidia kukuza kipato.

Alisema, mafunzo waliyopatiwa kabla ya kupatiwa mizinga hiyo, yatawaongoza katika uvunaji wa asali unaofuata kanuni na taratibu ambao utawawezesha asali yao kuwa na soko ndani na nje ya nchi.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa kuta za ukingo wa Mto Ng'ombe, eneo la Kijitonyama Ali Maua, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanamke aliyetupa kichanga choo cha halmashauri asakwa

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

JESHI la Polisi mkoani Kigoma linamtafuta mwanamke aliyetupa kichanga kinachokadiliwa kuwa na umri wa miezi minne hadi mitano katika choo cha Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/ Ujiji.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoa wa Kigoma, Alchelius Mtalemwa, alisema baada ya kupata taarifa za kukutwa kwa kichanga chooni, walifanikiwa kukichukua na kukipeleka kufanyiwa uchunguzi. "Wale ambao walikuwa wajawazito kwa maeneo ya hapa na hata maeneo mengine tutafuatilia kujua maeleezo ya kwa nini ujauzito umepotea," alisema.

Aidha, Mutalemwa amemtaka mhusika kujisalimisha mwenyewe katika vyombo vya usalama ili jamii ifahamu kitu gani kinaendelea kabla jeshi hilo halijatumia nguvu zaidi.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Shaban Magolwa, alisema uchunguzi umeonyesha kuwa tukio hilo limetekelezwa ndani ya saa 12 hadi 14 kabla ya mwili huo kubainika kwa kuwa kiumbe hakijabadilika sana.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Salvina Ishengoma, alisema wamepokea tukio hilo kwa masikitiko makubwa kwani limesababisha aibu kwa watumishi wa kike katika ofisi ya halmashauri hiyo.

Alisema jambo hilo linapaswa kukemewa na kuchukuliwa hatua kwani amekatisha uhai wa maisha ya kiumbe alichopewa na Mungu, pia kuaibisha jamii ya watumishi wa hamashauri hiyo.

"Yaani mtu unakuja kutenda tukio la kikatili katika vyoo vya umma, ilitakiwa baada ya kupata ujauzito akubaliane na hali yake," alisema.

# Mbatia awakaribisha waasisi wa NCCR-Mageuzi kurejea

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amewaalika vigogo na waliokuwa waasisi wa chama hicho, kurudi na kurejesha kasi ya kisiasa iliyokuwapo awali.

Mbatia amesema kama kulikuwa na makosa yaliyofanyika na kusababisha waasisi na vigogo hao wa zamani wa chama hicho kuondoka, tayari wamejifunza na kuyarekebisha na kwamba hayatajirudia tena.

Alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema mwaka huu wamejipanga kukirejesha chama hicho katika misingi yake ya awali na kasi zaidi.

Pia, alisema tayari baadhi ya watu wakiwamo wabunge waliowahi kuwa katika chama hicho wameomba kurudi na kwamba bado nafasi ipo ya kuwapokea watu mbalimbali waliowahi kujiunga na chama hicho na ambao hawajawahi kuwa wanachama.

"Wale wote waliotoka NCCR-Mageuzi wakiwa waasisi wa mageuzi, tunaomba warudi nyumbani, kwa sababu huku ndiyo nyumbani kwao, sisi tukiwa kama waasisi wa mageuzi tumeshajifunza na tunasema makosa yetu ya jana ambayo tulifanya yaliyowasikitisha sana ni mafundisho yetu ya leo, na tunawaambia kwamba tayari tumeshajifunza na hayatajirudia tena," alisema Mbatia na kuongeza:

"Na kama tuliwakosea tunawaomba radhi kweli kweli, warudi nyumbani, nguzo tuliyosimika ya uasisi wa mageuzi iendelee na tushiriki kwenye nafasi zote za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kuanzia nafasi ya urais Zanzibar na Bara, wabunge wa baraza la wawakilishi, wabunge wa Jamhuri ya Muungano na madiwani."

"Waasisi wale walioweka damu na jasho lao katika mageuzi, tunaomba mrudi, tunajua kuna wabunge na madiwani ambao wameshaomba kurudi nyumbani, tunawakaribisha tunaomba warudi tu, na pia kuna kundi la vijana wa kizazi kipya wameomba kujiunga nasi, nao tunawakaribisha sana."

Alisema tayari anaanza ziara ya kuzunguka katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuzungumza na wanachama katika mikoa hiyo ikiwamo kufungua matawi katika mikoa hiyo.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Mbatia alimpokea na kumkabidhi kadi ya chama hicho aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), Edward Simbeye, ambaye amejiunga na chama hicho.

Akizungumza katika mkutano huo baada ya kukabidhiwa kadi, Simbeye alisema kilichomsukuma kujiunga na chama hicho ni kutokana na kanuni na miongozo mizuri iliyopo kwenye katiba ya chama hicho.

"Katiba ya NCCR-Mageuzi imeeleza kwa kina nini maana ya utu, niwaombe vijana wenzangu popote walipo wajiunge na chama kinachojali utu wa mwanadamu, twende tukakijenge chama na nchi yetu, naamini kwamba chama hiki kinawajenga vijana kubishana kwa misingi ya hoja, bila matusi wala kejeli wala kutishia kufanya vurugu, mambo ambayo ni muhimu katika kuifikisha nchi yetu kule tunakotaka," alisema Simbeye.

mwisho

# Majaliwa: Maeneo ya shule yatumike kitaaluma

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amepiga marufuku shughuli zisizohusiana na taaluma kama ujenzi wa viwanda katika maeneo ya shule ili kutoa fursa kwa wanafunzi kuwa kwenye mazingira mazuri ya kujifunzia.

"Sheria inakataza kuweka matumizi yoyote yasiyokuwa ya kitaaluma katika maeneo ya shule kwani yanasababisha kelele hivyo wanafunzi kushindwa kusoma vizuri."

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi jioni baada ya kupokea malalamiko ya wazazi kuhusu eneo la Shule ya Msingi Mshikamano iliyoko Halmashauri ya Mji Handeni mkoani Tanga kuuzwa kwa mfanyabiashara, ambaye amefungua karakana ya kutengeneza magari.

Kufuatia hali hiyo, Waziri Mkuu aliuagiza uongozi wa halmashauri hiyo ukazungumze na mfanyabiashara huyo ili aondoe karakana katika eneo hilo, na kumtafutia eneo mbadala kwa ajili ya kuendesha shughuli zake na eneo hilo libaki kwa ajili ya masuala ya kitaaluma.

Pia, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Handeni upange matumizi bora ya ardhi kwa kuainisha maeneo ya makazi, biashara, viwanda na huduma za kijamii ili kuepuka mji huo kujengwa bila ya mpangilio.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwataka wananchi kuwafikisha kwenye vyombo vya dola walimu watakaobainika kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi. "Serikali imeweka sheria kali ya kumlinda mtoto wa kike, ukimpa mimba, ukimchumbia au kumuoa adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela."

Akizungumzia kuhusu uwapo wa mabango mengi kwenye mikutano ya hadhara ya viongozi wa kitaifa, Waziri Mkuu alisema kunadhihirisha wazi kwamba watendaji wa halmashauri hawawatembelei wananchi katika maeneo yao na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.

"Watendaji hamuendi kuwatembelea wananchi na kusikiliza matatizo yao, haiwezekani wawe wanawasubiri viongozi wa juu na kuwasilisha kero zao, sasa jipangeni haya mabango yote mtakuja kuyajibu kwa sababu hoja zote ni za ngazi ya halmashauri," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali imeelekeza nguvu kubwa katika kuwatumikia wananchi na kutatua kero zao, hivyo itasimamia kuhakikisha kila mtumishi anawajibika kwa kiwango kinachostahili.

"Serikali hii haimlindi mfanyakazi ambaye ni mbadhirifu, mwizi na asiyefanya kazi kwa weledi au anayebagua wananchi eti kwa uwezo wake wa kifedha au rangi au dini yake au chama chake. Hivi vitu havipo katika serikali kila mwananchi aliyeko Nzega anatakiwa kuhudumiwa," alisisitiza.




Ofisa Programu Mwandamizi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyohusisha vituo vya taarifa na maarifa vya Wilaya ya Ilala ambavyo viko chini ya mtandao huo jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Kibiti yapewa mashine 48 za makusanyo ya mapato

**Na Yasmine Protace,** KIBITI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, imepatiwa na serikali mashine 48 za kutunzia kumbukumbu za mapato yanayokusanywa katika vijiji.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Khatibu Chaulembo, katika kikao cha robo mwaka cha Baraza la Madiwani.

Chaulembo alisema kuwa kutolewa kwa mashine hizo katika vijiji ni msaada tosha ambao utawezesha kufahamu kinachopatikana kupitia makusanyo ya mapato.

"Tumepatiwa mashine 48 katika vijiji, ambazo zitatusaidia kuhifadhi kumbukumbu za mapato ambayo tutakuwa tunayakusanya kupitia vyanzo vyetu vya mapato," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa kinachotakiwa ni kuwapo kwa ubunifu, ambao utasaidia kusimamia miradi na kama ubunifu hautakuwapo, mapato hayawezi kuongezeka, licha ya kuwa yatakuwa yanakusanywa.

Kwa mujibu wa Chaulembo, kama mapato hayatasimamiwa vizuri, halmashauri haziwezi kuendelea.

Aliongeza kuwa serikali za vijiji haziwezi kuendelea bila kuwa na fedha, hivyo inatakiwa kusimamia miradi na mapato ili kuleta maendeleo katika sehemu husika.

# Mkemia Mkuu ataka mjadala udhibiti kemikali

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amezitaka taasisi za udhibiti wa kemikali na wadau kujadili namna bora ya kusimamia na kudhibiti kemikali zinazoharibu tabaka la hewa kulingana na mkataba uliosainiwa na nchi.

Mkataba huo wa kimataifa ulisainiwa mwaka 1987 kwa lengo la kulinda tabaka la hewa kwa kuondoa uzalishaji wa kemikali na vitu ambavyo vinaharibu tabaka hilo ambalo huzuia athari za mionzi ya jua kufika moja kwa moja duniani.

Mkataba huo ulianza utekelezaji rasmi Agosti 26, 1989 na Tanzania iliridhia mkataba huo mwaka 1993.

Mkemia Mkuu wa Serikali alitoa wito huo, jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua kikao cha pamoja kati ya Mamlaka za Udhibiti wa Kemikali hizo na wadau kwa ajili ya kujadili namna ya kuimarisha udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la hewa.

"Naelewa majadiliano ya kikao hiki yanalenga kuweka utaratibu wa kuboresha utekelezaji wa mkataba wa makubaliano ya Montreal ya mwaka 1987 ikizingatiwa kuwa kemikali chini ya protokali hiyo zinatakiwa kufikia ukomo wa matumizi yake mwaka 2030.

Najua mtapata uelewa wa majukumu ya kila taasisi inayohusika na mkataba huo ndani ya serikali pamoja na wajibu wenu nyinyi kama wadau mnaojishughulisha na kemikali hizo," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema katika kikao hicho watajadili kwa pamoja namna ya kuanza kupunguza kiasi cha uingizaji wa kemikali hizo kufikia mwaka 2030 na zitaondolewa kabisa katika matumizi na kusitishwa uzalishaji wake.

"Ni imani yangu mtajikita katika kuweka msisitizo wa kupunguza na kukomesha uagizaji wa kemikali hizi kwa lengo la kuweka mazingira ya nchi yetu salama dhidi ya uharibu wa tabaka la hewa la ozone," alisisitiza Dk. Mafumiko.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Kemikali nchini, Daniel Ndiyo, alisema kikao hicho kimehusisha pia wadau kwa lengo la kujadili kwa pamoja na kukubaliana utaratibu utakaotumika ili kuimarisha utekelezaji wa mkataba huo unaosimamia kemikali zinazoharibu tabaka la hewa.

Alisema mjadala huo utajikita katika kutengeneza na kukubaliana utaratibu wa kupunguza uingizaji na utumiaji wa kemikali hizo ili ifikapo mwaka 2030, kemikali hizo ziwe zimeondolewa katika matumizi na mbadala wake ndio uwe unatumika.

Baadhi ya kemikali ambazo zinahusishwa na uharibifu wa tabaka la hewa ni kama chlorofluorocarbons (CFCs), hydro chlorofluorocarbons (HCFCs), halons, methyl bromide, carbon tetrachloride, hydrobromofluorocarbons, chlorobromomethane, and methyl chloroform ambazo hutumika kama gesi za kwenye magari na friji.

# BoT yaja na mfumo bora wa uwekezaji taasisi, mashirika

**Na Allan Isack,** ARUSHA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema imeandaa mfumo bora wa kuziwezesha taasisi binafsi na mashirika ya umma kuwekeza kwa faida badala ya kupata hasara katika shughuli za biashara na uwekezaji kwenye jamii.

Akizungumza wakati wa semina ya waandishi wa habari za uchumi na biashara, Meneja wa Idara ya Masoko na Fedha wa BoT, Tawi la Arusha, Lameck Kakulu, alisema kuwekeza kuna faida kubwa kwa kuwa mwekezaji ana fursa ya kujipatia faida kuliko hasara.

Alisema kiwango cha riba kwenye dhamana za muda mfupi kilishuka kutoka asilimia 8.5 Agosti hadi asilimia 5.5 Desemba mwaka 2019.

Hata hivyo, alisema matokeo ya utekelezaji wa sera bora za fedha iliongeza ujuzi wa fedha kwenye benki kutoka wastani wa asilimia saba hadi nane.

Aidha, alisema benki za biashara ziliongoza ushiriki kwenye uwekezaji wa dhamana ya serikali kwa asilimia 67 na kwa upande wa mifuko ya pensheni, dhamana ilipanda kutoka asilimia nane hadi asilimia 20.

Pia alisema ushiriki wa wawekezaji binafsi dhamana ilipanda kutoka asilimia mbili hadi kufikia asilimia sita.

Aidha, alisema uwekezaji katika soko la upili zimeendelea kukua na dhamana ya muda mrefu imefikia thamani ya Sh. bilioni 815.70 na ziliuzwa na kununuliwa, ukilinganisha na kipindi kilichopita thamani hiyo ilikuwa Sh. bilioni 203.99.

Alisema ongezeko hilo lilitokana na kurejea sokoni kwa mifuko ya pensheni pamoja na kuongezeka kwa uelewa kwa wawekezaji wa mashirika na taasisi binafsi.

Kakulu alisema kiwango halisi cha dhamana za muda mfupi na muda mrefu kilichopatikana ni Sh. bilioni 2,572.52 sawa na asilimia 103, wakati kiwango



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Mkoa wa Arusha, Yasmini Bachu (kulia), akitoa mafunzo ya kutengeneza mitandio ya batiki wakati wa uzinduzi wa kikundi cha Binti CCM, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mil.10/- kutumika kuchanja mifugo

**Na Jaliwason Jasson,** HANAN'G

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hanan'g mkoani Manyara, inatarajia kutumia Sh. milioni 10 kwa ajili ya chanjo ya ng'ombe ili kuiepusha mifugo hiyo na magonjwa mbalimbali.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Bryson Kibasa, wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

"Tunatarajia kutumia kiasi cha Sh. milioni 10, kwa ajili ya kutoa chanjo kwa ng'ombe ili kuwaepusha na magonjwa mbalimbali," alisema Kibasa.

Hoja ya mifugo kupewa chanjo ilibuliwa na madiwani hao sambamba na kuitaka halmashauri hiyo kufanya sensa ya kutambua mbwa waliopo kwenye eneo hilo.

Hata hivyo, hoja ya kufanyika kwa sensa ya kutambua mbwa waliopo kwenye eneo hilo ilipingwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, George Bajuta.

Aidha, Bajuta aliwataka wananchi kuwachanja mbwa wao na kuwafunga nyakati za mchana.

"Wataalamu watembelee wafugaji kuangalia kama wananchi wanachanja mbwa wao, ni vizuri katika halmashauri yetu kila mbwa achanjwe," alisema Bajuta.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, aliliambia baraza hilo kuwa mpango uliopo kwa sasa ni kuhakikisha wanachanja ng'ombe zote katika eneo hilo.

Aliwaagiza wataalamu wa mifugo kuharakisha mpango wa kuchanja ng'ombe.

Mkazi wa Dirma, Issaay Boay, alisema ni vizuri wafugaji wa mbwa wakapewa elimu ya kuwatunza kuliko kuwaua.

John Saitoti, mkazi wa Katesh, alisema mbwa wanaozurura ni haki kupigwa risasi ili wasilete madhara kwa kung'ata watu husussan watoto.

Akizungumzia suala la serikali kuchanja ng'ombe, alisema ni

## Mbarawa awaelekeza viongozi usimamizi maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, amewataka viongozi wilayani Monduli, kusimamia na kulinda miundombinu ya maji, na kutoa taarifa za watu wanaoharibu miundombinu hiyo, ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Akizungumza jana katika ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya maji Wilaya ya Monduli, Prof. Mbarawa, alisema kuna baadhi ya miradi ya maji imeharibiwa na wananchi kwa kukata mabomba, hivyo wameisababishia serikali hasara. Hata hivyo, alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi ya maji, hivyo vema kwa viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia na kuilinda miradi hiyo, kukamata watu wanaohusika kuharibu miundombinu ya maji.

"Mradi wa Monaro unaunganisha Kata ya Moita na una chanzo kirefu cha maji, ambacho kinazalisha lita 18,000 kwa saa, lakini kuna tatizo la wananchi kukata mabomba ya maji bila kutambua kuwa serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi, sasa naagiza viongozi nendeni mkasimamie mradi huu, na mkikamata mtu mchukulieni hatua kali za kisheria," alisema.

Kadhalika, alisisitiza kutunzwa kwa miundombinu hiyo, kwa kuwa serikali imetumia gharama kubwa kujenga ili wananchi wapate huduma ya majisafi na salama.

Naye Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) Wilaya ya Monduli, Neville Msaki, alisema mradi huo una tatizo la usimamizi hafifu, hali iliyosababisha kushindwa kukarabatiwa kwa miundo mbinu hiyo.

"Mradi huu unashindwa kutoa huduma katika Kata ya Moita, kutokana na kutofanyiwa ukarabati wa makorongo na kusababisha maji kupotea… ili mradi ulete matokeo yaliyokusudiwa, ni lazima kulinda maji yasipotee kwenye makorongo, nashauri tubadilishe mabomba ya plastiki na kuweka ya chuma kwa gharama ya Sh. milioni 305," alishauri Msaki.

Diwani wa Moita, Prosper Meyan, alisema mradi huo kwa jamii ya kifugaji ni mgumu kutokana na kutumia gharama kubwa ya umeme kusukuma maji. Alitoa rai kujengwa kwa tangi katika Mlima Dume kwenye mfumo wa mradi mkubwa wa maji wa Arusha. "Tukitumia chanzo kitakachoshusha maji kutakuwa na uwezekano mkubwa wa maji kufika kila kijiji kisichokuwa na maji," alisema.

Mkuu wa Wilaya Monduli, Iddy Kimanta, alisema hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wa vijijini siyo ya kuridhisha, kwa kuwa kati ya wananchi 164,213 wanaopata, maji ni 111,266 sawa na asilimia 67.78 kwa msimu wa kiangazi na masika ni asilimia 76.



# Upepo Same waharibu miundombinu Tanesco

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

UPEPO mkali uliovuma katika Kata ya Kihurio na Ndungu katika Tarafa ya Ndungu wilayani Same, umeharibu miundombinu ya Shirika la Umeme nchini (Tanesco).

Upepo huo umeangusha nguzo 10 za umeme na kusababisha kukosekana kwa huduma ya nishati hiyo kwa takribani siku nne mfululizo.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wakazi wa kata hizo wamelalamikia Tanesco kwa kuchelewa kutafuta ufumbuzi, na kwamba kuchelewa kutatua tatizo kumesababisha hasara kubwa hasa kwa wafanyabiashara.

Nipashe lilishuhudia katika Kata ya Kihurio, baadhi ya wafanyabiashara wanaouza vinywaji baridi na wenye mashine za kukoboa na kusaga wakishindwa kufanya biashara kutokana na kukosa umeme siku nne mfululizo.

Mmoja wa wafanyabiashara katika kata hiyo, Bakari Charles, kukatika kwa umeme katika kata hiyo limekuwa ni sugu kutokana na baadhi ya nguzo zinazosafirisha umeme katika eneo hilo nyingi zimeoza na mara kwa mara zimekuwa zikianguka.

"Tumechukua mikopo benki tumenunua hizi mashine za kukoboa na kusaga nafaka, lakini tumekuwa tukikwama kutokana na tatizo la umeme katika kata yetu... haipiti wiki mbili lazima umeme ukatike na hii inasababishwa na uchakavu wa nguzo, tunaomba tubadilishiwe nguzo zote ikiwezekana," alisema Charles.

Naye Monica Mshana, mfanyabiashara wa chakula na vinywaji baridi, aliomba serikali kuingalia kata hiyo kwa jicho la pelee kutokana na kuwa pembezoni kwa kulimaliza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara.

"Vinywaji vingi vinavyopendwa na wateja ni baridi sasa, umeme unakatika kila wakati unategemea tunafanye biashara ya vinywaji, tumeshafikisha sana haya malalamiko kwa uongozi wa Tanesco, lakini ndio hivyo kama unavyoona leo siku ya nne hatuna umeme," alisema Monica.

Diwani wa Kihurio, Mariane Abraham, alisema tatizo la umeme katika eneo hilo limekuwa sugu kwa muda mrefu, hali ambayo imekuwa ikiwasababishia hasara wajasiriamali na wafanyabiashara wanaotegemea nishati hiyo kwa ajili ya kujiingizia mapato.

Naye Balozi wa Utalii na Maliasili ambaye ni mdau wa maendeleo katika kata hiyo, Nangasu Wallema, aliiomba serikali kumaliza tatizo hilo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika eneo hilo kwani linawakatisha tamaa na kurudisha nyuma shughuli za maendeleo.

Meneja wa Tanesco wa Kituo cha Ndungu kinachosimamia kata hizo, Abdallah Kondo, alisema sababu kubwa ya nguzo hizo nyingi kuanguka imetokana na kuoza.

Alisema utatuzi wa tatizo hilo utategemea namna Tanesco itakavyopata nguzo mpya.

# DC aitisha kikao cha dharura cha corona

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, ameitisha kikao kazi cha dharura na watendaji wa kata na vijiji katika Mji Mdogo wa Himo ili kutoa maelekezo ya kuwatambua wageni wanaoingia wilayani humo wakitokea Kenya.

Warioba amewataka viongozi hao kutoa elimu kwa wananchi na kuchukua tahadhari dhidi ya mwenendo wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na kirusi cha corona. Mkuu huyo wa Wilaya juzi alikutana na viongozi hao.

"Ndugu zangu watendaji wa kata na vijiji katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo na wale mnaotoka Tarafa za Vunjo Magharibi na Vunjo Mashariki, nimewaiteni hapa tupeane maelekezo kuhusu ugonjwa wa corona. "Niwaeleze wazi kwamba ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona ni hatari sana, lazima tufuate ushauri uliotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuepuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana.

Lazima kila mmoja wetu abadilike na tusiishi kwa mazoea." Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matibabu na kipokea washukiwa wa ugonjwa huo nchini ni pamoja na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Hospitali ya kudhibiti magonjwa ambukizi ya Buswelu ya Mwanza na Hospitali ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Inaelezwa kuwa ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.

Kulingana na taarifa rasmi kutoka Shirika la Afya Ulimwenguni, tangu mlipuko wa ugonjwa huo uanze katika mji wa Wuhan uliopo Jimbo la Hubei nchini China mwezi Desemba 2019 hadi 28 Januari 2020, jumla ya watu 4,593 wamethibitishwa kuugua ugonjwa huo duniani kote.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kibosho Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Elisha Moses (kushoto), akipongezwa na Matroni wa Shule ya Sekondari ya Manushi, baada ya kutangaza vita dhidi ya waendesha pikipiki wanaowapa lifti wanafunzi kwenye kata hiyo, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Uuzaji holela petroli, dizeli marufuku Same

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

SERIKALI ya Wilaya ya Same, imepiga marufuku uuzaji wa mafuta ya petroli na dizeli kwa njia za kienyeji katika maeneo yote ya vijijini.

Uamuzi huo unatokana na taarifa za kuwapo kwa watu watano wanaodaiwa kupoteza maisha kutokana na kuhifadhi petroli kwenye ya makazi yao.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, amethibitisha kuwa watu hao walipoteza maisha baada ya kuweka ndani ya nyumba mafuta hayo, kwa ajili ya kuwauzia madereva wa pikipiki wanaosafirisha abiria maarufu kama bodaboda.

Senyamule alisema watu hao watano waliofariki ni pamoja na mfanyakazi mmoja wa serikali, baada ya kushindwa kujiokoa na kulipukiwa na moto huo uliotokana na mafuta ya petroli.

Alisema kutokana na kuendelea kuibuka kwa matukio hayo, serikali imeagiza watendaji wa kata na vijiji kusimamia marufuku hiyo.

"Ni kweli nimepiga marufuku uuzaji holela wa petroli, na nimewataka wanaotaka kufanya biashara hiyo kufuata taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

"Kama wanataka kuendelea na biashara yao, wajenge vituo vya gharama nafuu vya kuuzia mafuta katika maeneo ambayo hayana vituo vikubwa vya kuuzia mafuta."

"Ninatoa onyo kwa wafanyabiashara wanaouza mafuta kwenye madumu na zile chupa za maji kuacha mara moja... kama wanataka kufanya hivyo biashara wawasiliane na Ewura kwa ajili ya kupata elimu juu ya ujenzi wa vituo vidogo vya gharama nafuu vya kuuza mafuta, vinginevyo kuanzia sasa tutafanya operesheni za kustukiza na tukiwakamata sheria itachukua mkondo wake," alisema. Mmoja wa wafanyabiashara wanaouza mafuta hayo ya vidumu katika Kijiji cha Saweni, Frank Sadic, alisema hawapingani na agizo la serikali, lakini wao wanatoa huduma hiyo kutokana na eneo kutokuwapo kwa kituo chochote cha kuuza petroli, huku kukiwa na vyombo vya moto kama bodaboda ambazo zinahitaji mafuta hayo.

Aliomba serikali kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wafanyabiashara wa maeneo ya vijijini ili waweze kujenga vituo hivyo vya kuuzia mafuta vya gharama nafuu ili kufanya biashara hiyo kwa kufuata sheria na kuondokana na ajali za milipuko ya moto inayogharimu maisha ya watu

Meneja wa Ewura Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Lorivil Long'idu, alisema wameanza kutoa elimu kwa ajili kupunguza matukio ya moto unaosababishwa na uuzaji holela wa petroli kwenye mapipa na madumu ya plastiki unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara hasa katika maeneo ya vijijini ambako hakuna vituo vya mafuta.

Alisema Ewura Kanda ya Kaskazini imeanza kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa petroli wenye mitaji midogo na wasio na uelewa wa kutosha juu ya ujenzi wa vituo rafiki vya gharama nafuu katika maeneo ya vijijini, na wengi wao wameitikia wito huo kwa kuanza ujenzi.

ama

ALHAMISI MACHI 5, 2020

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

**Aomba radhi kanisa lake kueneza corona**



Ukurasa 17

Ni vita ya aina yake kurekebisha walionasa na dawa za kulevya



Ukurasa 20

**Staili 'namba mbili' kukabili hodi ya corona barani Afrika**



## BAADA MIAKA 11...

# Simulizi za mwanasheria William ukomo mauaji ya wenye ualbino

Ukurasa 18



Lee Man – hee, akipiga magoti kuomba radhi. **PICHA: MTANDAO.**

## Aomba radhi kanisa lake kueneza corona

**Seoul,** Korea Kusini

KIONGOZI wa kidini nchini Korea, Lee Man – hee, ameomba msamaha kwa umma wa nchi yake, kutokana na eneo lake la imani kuwa mhusika mkuu aliyesambaza maradhi ya corona.

Lee ni kiongozi wa kanisa linalojulikana 'Shincheonji Church of Jesus' alifanya hivyo, huku akidhihirisha kauli yake kwa kupiga magoti.

Hadi sasa, asimilia 60 ya wanaougua corona idadi yao ni wastani watu 4,000 wana mzizi wa kanisani kwake na duniani nchi hiyo inashika nafasi ya 28 kwa kuwa na wagonjwa wengi.

Wakati China ambako ndiko kwenye mzizi kunaongoza kwa wagonjwa wengi duniani, idadi ya wanaougua dunia nzima inakadiriwa kuwa 90,000 wiki hii.

Nchini Korea Kusini, athari zaidi ni katika mji wa Daegu, kunakochukua asilimia 75 ya wageni kwa wote katika nchi hiyo na theluthi tatu ya wagonjwa hao wanaelezwa wanatokea kanisani.

Kati mji Mkuu wa Seoul, ambao una wastani wa wakazi milioni 10 (mara mbili ya Dar es Salaam), hakujaingiliwa na Meya wake amekuwa akiwahimiza wakazi kuwa makini na mjumuiko wa makundi na inapobidi kubaki majumbani.

AFYA

# Shinyanga kinara kitaifa mimba ya mabinti kupitia matukio haya

• Babu miaka 70 vs binti miaka 14 • Ulimbukeni mahari ng'ombe sita • Shule kwa wasichana yabaki shubiri



Mkurugenzi wa Shirika la Agape, John Myola, akielezea wanavyosaidia waathirika wa mimba na ndoa za utotoni kutimiza ndoto zao, kwa kuwasomesha elimu ya watu wazima. **PICHA: MARCO MADUHU.**

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

TATIZO la mimba na ndoa za utotoni Shinyanga limebaki kuwa sugu. Inawahusu wote walioko shule na hasa sekondari.

Kuna wanaoozeshwa ili wazazi wapate mahari, hasa mifugo. Takwimu za kitaifa mwaka 2012, zinaonyesha Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora kuhusu madhara ya uozeshaji watoto (58%), kisha Mara (55%).

Mwathirika wa ndoa za utotoni (jina limehifadhiwa) mwenye umri miaka 16, mkazi wa Shinyaga Mjini, anasimulia alipomaliza darasa la saba alikuwa na miaka 14 na alipofaulu kuendelea na sekondari, bibi yake aligoma, badala yale alimuozesha akawe mke wa nne.

> **Walianza 2006, baada ya miaka sita, waligundua tatizo la mimba na ndoa hizo, hata mabinti wengi walishindwa kumaliza masomo.**

Anasema awali mwanamume alimpenda, lakini baada ya kupata mtoto wa kwanza, alianza kumnyanyasa akidai hamhudumii vizuri kama wake zake wengine, alimnyima hela za matumizi, ndipo alipoamua kuikimbia na mtoto aliumachia bibi yake.

"Siku moja nililisikia shirika la Agape likitoa elimu ya kupinga matukio ya mimba na ndoa za utotoni, huku likihitaji kusaidia waathirika wa matukio haya.

"Ikabidi nijitokeze na sasa wanasomesha kwenye shule yao ya mfumo wa elimu ya watu wazima. Nipo kidato cha pili na ndoto zangu ni kuja kuwa mwalimu," anasema mwanamke, huyo ambaye baba yake alishafariki.

Mwingine (jina limehifadhiwa) ana umri wa miaka 20, mkazi wa Kishapu, anasema aliozeshwa na baba yake mzazi alipomaliza darasa la saba, akiwa na miaka 14 kwa mahari ya ng'ombe saba, mumewe alikuwa na miaka 32 aliyemzalisha watoto wawili mfululizo.

Anasimulia kwamba, alishindwa kumudu familia na akakimbilia mjini Shinyanga kufanya kazi za ndani, ndipo alipokutana na shirika la Agape, lililomsomesha ufundi cherehani na sasa anajitegemea, akiwa katika hatua ya mbali ujenzi wa nyumba yake.

Mwingine, mkazi wa Kata ya Lubaga wilayani Kishapu mwenye miaka 14, anasema alikomea darasa la awali, baada ya baba yake kugoma kumsomesha. Aliambiwa 'ni wa kuolewa tu.'

Anasema, mwaka juzi alipokuwa na umri miaka 11, baba yake alimuozesha mume wa miaka 70 kwa mahari ya ng'ombe sita na alipogoma, binti anasimulia alipigwa na vitisho, kasha alipelekwa kwa mume kwa nguvu.

Msichana huyo anasimulia uzoefu wake, alipolala na mzee huyo, alitetemeka sababu hakuwahi kufanya tendo hilo, pia alipofanya iliambatana na maumivu makali, ili hakupata ujauzito, kabla mama yake kumuokoa.

"Mama yangu mzazi walitengana na baba. Nipo mimi pamoja na mdogo wangu wote wa kike, tukabaki kuishi na mama wa kambo ambaye naye alikuwa akishabikia niolewe kwa huyo mzee. Baada ya kuolewa kwa nguvu, ikabidi nitafute mawasiliano ya mama.

"Ndipo akaja kuniokoa na sasa naishi naye. Sina elimu yoyote, sijui kusoma wala kuandika. Nimebaki kukaa tu nyumbani, sababu ndoto zangu zimeshazimwa na sijui wapi pa kuanzia, nipo naishi na mama yangu mzazi, pamoja na mdogo wangu," anaeleza.

Mkasa mwingine unamhusu mwanamke aliyebakwa na shemeji yake na baada ya ujauzito, alifukuzwa nyumbani na dada yake, akidai ujauzito huo hakupewa na mume wake, pia shule akafukuzwa.

Anasema, alipojifungua alimuacha mtoto kwa mama yake mzazi, kisha akaenda kutafuta msaada kwenye shirika la Agape kuendelea na masomo ya sekondari, alikofanikiwa sasa yuko elimu ya watu wazima.

"Ndoto zangu ambazo zilizotaka kuzimika, sasa hivi zimeamka na zitatimia, sababu kwenye matokeo yangu ya kidato cha nne mwaka huu 2019, nimepata ufaulu wa daraja la pili na ninakwenda kidato cha tano na ninataka nifike hadi chuo, nataka kuwa mwanasheria," anaeleza.

### WAZAZI

Paulina Shija, mzazi mwenye mtoto aliyeumizwa na ndoa za utotoni, anasema uozeshaji watoto wadogo unasababishwa na mila zinazomtambua binti ni kitega uchumi, kupitia mahari ya mifugo.

Ana uzoefu binafsi mtoto wake wa kwanza aliolewa kwa mahari ya ng'ombe sita, lakini ndoa ilimshinda mtoto na aliamua kurudi nyumbani, ndoto za masomo zimezimika.

"Binti akishavunja ungo tu,

AFYA

# Shinyanga kinara kitaifa mimba ya mabinti kupitia matukio haya

tayari anaanza kutafutiwa mchumba, ili aolewe na kuleta ng'ombe nyumbani," anasema Shija.

Mzee Sonda Kabeshi wa Shinyanga, anasema mila na desturi za kabila la Wasukuma, mtoto wa kike anaingia katika orodha ya kuleta utajiri kwa familia na wa kiume anatajwa 'mfujaji mali.'

"Mtoto wa kike akishavunja ungo tu na kuchomoza matiti, tayari mzee anaanza kuhesabu hizo ni ng'ombe zinakaribia kuingia katika familia,,"anasema Kabeshi.

Ngassa Maganga, mkazi maarufu kijijini Mwamala, Shinyanga Vijijini, anazieleza mbinu za kukwepa makali ya sheria, wanamshawishi binti afanye vibaya masomoni, wao wanufaike na mahari ya ng'ombe.

"Pia taaluma yangu ni mwalimu nimestaafu mwaka 2016, haya ninayosema nina ushahidi nayo. Nimeshuhudia mabinti waliokuwa wazuri kweli kimasomo, wakifeli," anasimulia Mzee Maganga.

Pia, anataja umaskini wa familia kushindwa kumtimizia binti mahitaji, inamkatisha tamaa na anaamua kujiingiza katika mambo kinyume na staha zake, abahatishe mahitaji yake.



Paulina Shija, mkazi wa wilayani Kishapu, Shinyanga, akielezea alivyozimwa ndoto zake kwa ndoa ya utotoni. **PICHA: MTANDAO.**

### KAULI AGAPE

John Myola ni Mkurugezi wa Shirika binafsi la Agape, linalotetea haki za wanawake na watoto mkoani Shinyanga, anataja jukumu lao ni kuelimisha na kutokomeza mimba na ndoa za utotoni kwa waathirika, warudishe matumaini ya ndoto zao.

Anasema, walianza mwaka 2006 na baada ya miaka sita, 2012, waligundua tatizo la mimba na ndoa hizo, hata mabinti wengi walishindwa kumaliza masomo.

Myola anasema, walianzisha mradi wa kutokomeza matukio hayo, kupitia elimu katika jamii kuhusu madhara ya kuozesha watoto na uendekezaji mila kandamizi.

"Tulianza kwenye Kata mbili za mjini Shinyanga kama majaribio," anasimulia Myola na kuongeza walipanua na kuupeleka wilaya za Kishapu na Shinyanga Vijijini, walikobaini hali ngumu zaidi.

"Baada ya kuona tatizo ni kubwa zaidi, sanjari na kutibua ndoa za watoto hawa siku za harusi zao na kukosa mahali pa kuwapeleka, ndipo ikabidi tubuni mbinu ya kuishi nao kwenye shirika letu," anasimulia.

Anasema, katika kundi hilo wapo waliopatiwa elimu ya sekondari na wengine walichagua kusomea ufundi na walipelekwa katika vyuo husika.

Felex Ngaiza, ni Mwanasheria wa Agape, anayeelekezea lawama sheria ya ndoa iliyopo sasa, akidai imechangia vikwazo kuzuia ndoa na mimba za utotoni.

> **"Mama yangu mzazi walitengana na baba. Nipo mimi pamoja na mdogo wangu wote wa kike, tukabaki kuishi na mama wa kambo ambaye naye alikuwa akishabikia niolewe kwa huyo mzee.**

### OFISA SERIKALI

Tedson Ngwale ni Katibu Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Serikali wa Kupunguza Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa), Mkoa wa Shinyanga, anasema serikalini hivi sasa inapunguza mimba na ndoa za utotoni, kupitia elimu kwa jamii.

Anataja mkakati mingine ni ujenzi wa nyumba salama za kuhifadhi waathirika na mimba, pia ndoa za utotoni, ili kesi zinapoendeshwa wasirudi majumbani na wakarubuniwa.

Pia, anataja msako dhidi ya waganga wa kienyeji wanaorubuni kinamama kwa kuwatia hofu wasichana kuwapa dawa za mapenzi maarufu 'samba' na anafafanua:

"Mkoa tayari umeshaagiza wakuu wa wilaya wote pamoja na wakurugenzi kufanya msako wa waganga wa kienyeji ambao wanaogesha dawa za mapenzi watoto wa kike na kuleta orodha ya majina yao yote hapa mkoani, ili wapate kutambulika. Mkuu wa Mkoa atafanya mazungumzo nao na kuwapatia maagizo mazito,

"Pia, tunafanya mawasiliano na kampuni za simu za mkononi, ili kuwa zinatuma jumbe mfupi (sms) kwa wakazi wa Mkoa wa Shinyanga, zinazopinga matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambapo 'sms 'hizo moja ya kampuni za simu zimeshaanza kutuma," anaeleza.




Mwathirika wa mimba ya utotoni, akielezea simulizi anayodai udhalilishaji uliomkuta kutoka kwa mwalimu wake, akaangukia ujauzito na hatimaye kufukuzwa shule.

Anataja takwimu za ndoa za utotoni mkoa Shinyanga, kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2019 ni watoto 32 walio na umri chini ya miaka 18, huku kukiwapo mimba 168 za wanafunzi na wameshaacha masomo, wa shule za sekondari 167, msingi kuna mimba Saba.

AFYA

SHIDA VITAMBULISHO

# Wazee Kishapu 'watosa' hospitali warejea zama za tiba mitishamba



Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Rehema Kasita, akiwaeleza jambo wazee wa Kishapu, kuhusu vitambulisho vyao vya matibabu. **ZOTE: MARCO MADUHU.**

**Na Marco Maduhu, aliyekuwa Kishapu**

MZEE ni nani? Kisheria, hata kiafya, ni mtu aliyetimiza umri wa miaka 60.

Sera ya Wazee ya Mwaka 2003, inawapa haki ya kupatiwa huduma za afya bila ya malipo, katika vituo vyote vya afya vya serikali nchini.

Licha ya kuwapo haki hiyo kisheria, utekelezaji wake bado haujafika kiwango cha juu zaidi. Katika baadhi ya maeneo, wazee hao wanalazimika kuingia mifukoni kutoa fedha za matibabu.

**WAZUNGUMZA**

Wilayani Kishapu katika Mkoa wa Shinyanga, hiyo inaajiri zaidi. Wazee, wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa matibabu ya bure, sababu kuu ni kukosa vitambulisho vinavyowaidhinisha kupata huduma hiyo ya afya bure.

Ndulu Keneja, ni mkazi wa kijiji cha Kiloleli wilayani Kishapu, ambaye hana kitambulisho cha matibabu bure.

Anaeleza alivyo kiafya sasa, hana nguvu tena ya kufanya kazi za kumuingiza kipato na pale anapougua na kwenda hospitali kupatiwa matibabu, analazimika kutoa fedha zake mfukoni, baada ya kuuza mifugo yake.

Mzee huyo anasema, kuna wakati anapougua na kukosa fedha ya kwenda kupatiwa matibabu, analazimika kutumia dawa za jadi - mitishamba.

Ni dawa ambazo zinazalishwa kwa kuchemsha mizizi au matawi ya miti, kutokana na ugonjwa anaougua na hata kusaidia kupoza makali ya ugonjwa, hata akaendelea na maisha yake kila siku.

> Kuna baadhi ya magonjwa ya wazee hayaponi kwa mitishamba, bali yanaishia kupoza makali tu ugonjwa, jambo wanalofahamu, lakini hakuna mbadala wake.

Pia, Mzee Keneja, anasema kuna baadhi ya magonjwa ya wazee hayaponi kwa mitishamba, bali yanaishia kupoza makali tu ugonjwa, jambo wanalofahamu, lakini hakuna mbadala wake.


"Wazee wengi tu kwenye wilaya hii ya Kishapu hawana vitambulisho vya matibabu bure nikiwamo na mimi na pale tunapokosa huduma za matibabu kwenye huduma za afya, inatulazimu turudi kwenye zama zetu za zamani za kutumia dawa asili za mitishamba, ili kupoza makali ya magonjwa

"Mfano mimi mwenyewe pale ninapokuwa naugua na kujikuta mfukoni sina hela ya kwenda hospitali kupatiwa matibabu, huwa nachimba mizizi ya miti, ukiwamo mwarobaini, nachemsha kisha na kunywa pamoja na wajukuu zangu. Magonjwa mengine kama malaria huwa tunapona kabisa," anaongeza.

Mzee Emmauel Lufyekela, mkazi wa Bunambiu wilayani Kishapu, anasema wazee wengi wanakabiliwa na magonjwa ya kizee kutokana na umri wao, akitaja baadhi kuwa ni shinikizo la damu, tezi dume, kisukari, kibofu cha mkojo, magonjwa ambayo hayatibiki kwa mitishamba, bali dawa za hospitalini.

**MWENYEKITI WAZEE**

Mwenyekiti wa baraza la Wazee wilayani Kishapu, Suzana Masebu, anasema wengi wilayani humo hali zao ni duni, kutokana na ujana wao walijishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji na baada ya kuzeeka nguvu zinawaishia, hawamudu tena kujiingizia kipato.



Mzee Bundala Salehe kutoka Shangihilu wilayani Kishapu, akitoa neno kuhusu adha ya kutopata matibabu bure, chanzo ni kukosa kitambulisho.

Anasema, kwa mila za kabila lao wasukuma, wazee wanapenda kuishi na wajukuu zao na kujikuta hata ile mifugo aliyokuwa akiitengemea kuendesha maisha ya uzeeni, inamalizwa na wajukuu.

Hivyo, anasema wanajikuta wameshapoteza mali na kuwafanya waanangukia katika za maisha ya umaskini na kutokana na hilo, wao Baraza la Wazee wamekuwa wakijitahidi kushirikiana na mashirka ya kutetea haki za wazee kuwasaidia.

Pia, serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, ilitenga bajeti kwa ajili ya kuwakatia vitambulisho wazee wapate matibabu bure, ili kuwaondolea changamoto ya matibabu.

"Wazee ambao hawana vitambulisho hivi vya matibabu bure, wamekuwa wakipata tabu ya kupatiwa matibabu bure kwenye huduma za afya na hata kama wakihurumiwa huishia kwenye vipimo tu, huku wakiambiwa wakanunue dawa na wakati hata pesa hawana, hivyo kurudi kutumia dawa asili za mitishamba.

"Sera hii ya Wazee ya Mwaka 2003, ili ipate kutekelezeka kwa vitendo katika utoaji wa huduma za matibabu bure kwa wazee, lazima itungiwe sheria ili kila kitu kiwe kinatekelezwa kwa mujibu wa Sheria," anafafanua Suzana

**USTAWI & MAENDELEO**

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Rehema Kasita, anataja takwimu za wazee wilayani kuwa jumla yao wapo 15,462, wanawake 8,462, na wanaume 7,000. Katika orodha hiyo, walio na vitambulisho vya matibabu bure wako 12,148.

Anasema kilichowakwamisha wazee 3,314 wasiwe na vitambulisho vya matibabu bure, ni ufinyu wa bajeti katika halmashauri yao.

Rehema anatumia fursa hiyo akiahidi fedha zikapopatikana, hao waliobaki watakatiwa vitambulisho vitakayowandolea adha hiyo ya ukosefu wa matibabu bure kwenye huduma za afya.

"Ni kweli bila ya kuwa na kitambulisho hicho huwezi kupewa huduma ya matibabu bure, kwa sababu serikali haikutambui. Hivyo, nawaomba wazee wangu tuvumiliane pale pesa itakapopatikana, tukawakatia wote," anasema.

Joseph Swalala, ni Mkuu wa Idara ya Maendeleo katika Halmashauri Wilaya Kishapu, anayewatoa hofu wazee hao, kwa ahadi serikali itaendelea kutatua changamoto zinazowakabili wazee, hasa kwenye huduma za afya mahsusi katika tiba, upatikanaji dawa, madirisha na madaktari maalum kwa wazee.

Anasema, ni moja ya sababu halmashauri hiyo imeongeza mabaraza ya wazee kutoka katika kata mbili hadi 17, za sasa. Kishapu ina jumla ya kata 29, lengo ni kubaini changamoto zinazowakabili, kisha kutatuliwa.

Kwa mujibu wa Swalala, hadi sasa suala hilo la vitambulisho vya matibabu bure, limeshaingizwa tayari kwenye mkakati wa bajeti ya halmashauri.

**NGO WASHIRIKI**

Kaimu Mratibu wa shirika lisilo la kiserikali la Tawale, linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga, Judith Kalwani, anasema hivi sasa wanaendesha mradi wa kufanya mifumo ya utawala, ili kuwajibika kwa wazee.

Anafafanua kwamba, hiyo inahusu masuala ya wazee kwenye mipango yao ya bajeti, ili kutatua changamoto zao zikiwamo za matibabu.

Judith anasema mradi wao wanaoutekeleza katika halmashauri za Kishapu na Kahama Mjini, ulianza Agosti 2019 na utakoma Julai mwaka huu, wakilenga kutatua changamoto zinazowakabili wazee, hasa suala la kupata matibabu bure, eneo ambalo wengi wanapoteza maisha kwa sababu za kukosaa fedha za matibabu.

"Tumekuwa tukitekeleza miradi mbalimbali ya kusaidia wazee kuondokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili, ikiwamo kutokomeza mauaji ya kishirikina, eneo ambalo tumefanikiwa. Sasa tupo kwenye uboreshaji huduma za afya kwa wazee.

"Asilimia 96 ya wazee wamekuwa wakiishi maisha magumu kutokana na hapo awali hawakuwa na ajira rasmi na kutokuwa na mafao, ambayo yangeweza kuwasaidia kidogo kiuchumi na asilimia nne ndio waliokuwa na ajira rasmi, sababu ambayo imekuwa ikichangia wazee wengi kukosa fedha za matibabu,

> Tumekuwa tukitekeleza miradi mbalimbali ya kusaidia wazee kuondokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili...

"Sisi kama shirika tunahamasisha serikali kupitia kwenye halmashauri iwe inatenga bajeti za wazee, ili wapatiwe vitambulisho bure vya matibabu, kwa sababu kila mwaka huwa kuna ongezeko la wazee wapya, ambao wanafikisha umri wa miaka 60 na wanatakiwa waingizwe kwenye msamaha wa matibabu," anafafanua.

Oktoba Mosi ya kila mwaka, dunia huadhimisha Siku ya Wazee Duniani na nchini mwaka jana kitaifa, yalifanyika katika Uwanja Nangwanda Sijaona, mkoani Mtwara.

Mgeni rasmi Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema suala la utoaji huduma kwa wazee, limo katika orodha ya vipaumbele vya sasa vya serikali, kwa kuendelea kuboresha hali yao ya maisha, ikiwamo katika huduma za afya.

# Ni vita ya aina yake kurekebisha walionasa na dawa za kulevya



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi na Dawa ya Kulevya, walipowasilikiza waraibu wa dawa ya kulevya katika kituo cha matibabu yao, cha Itega, Jijini Dodoma. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace**

DAWA za kulevya zinaendelea kuwaharibia maisha watumiaji wake kila kukicha. Si nchini pekee, bali kimataifa, nguvukazi za vijana zinapotea

Wengi wanajiingiza kutumia bila kujua, inapokuja suala la kujiondoa, uhakika haupo.

Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa vijana jinsi ya kujikinga na dawa hizo, hata asasi binafsi nazo hazipo nyuma kisaidia; hapo kuna kuzungumza na vijana jinsi zilivyo athari za dawa za kulevya na zaidi ya hapo.

Hadi sasa kuna vituo na taasisi za watu binafsi, zinazowahudumia waathirika, baadhi wanaelezwa kupiga hatua ya 'kujikubali' wakipata dawa zinazowawezesha kurudia hali zao za kawaida.

Pia, wapo waathirika wasio na elimu yoyote kuhusu athari za dawa. Hao wanangukia mustakabali wa kuzidi kudhoofu kiafya, maana hawako katika mkakati wa kujinusuru.

Hivi karibuni, serikali iliihakikishia Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi na Dawa ya Kulevya, kwamba itaendelea kuboresha huduma kwa waathirika wa dawa, kupitia tiba inayoitaja dawa ya Methadone.

Mkurugenzi wa Idara ya Kinga katika Wizara ya Afya, Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, anaiambia Kamati ya Bunge chini ya Oscar Mukasa, katika ziara waliofanya kwenye Kituo cha Kuhudumia Waathirika cha Itega, jijini Dodoma.

Dk. Subi anasema, serikali inatarajia kufungua kituo cha Methadone mkoani Tanga mwezi ujao, akifafanua vita ya dawa ya kulevya, inahitaji ushirikishaji wa sekta mbalimbali na ndio sababu wanatumia asasi zisizo za serikali kuwafikia watumiaji na kuwaleta vituoni.

"Imesaidia sana kuwajenga kijamii na ndio maana kuna wengine wanasema ndoa ziliisha lakini kwasasa wanaishi na wake zao" anasema Dk. Subi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Oscar Mukasa, anaishauri serikali kuwa makini na kuwapo kiwango kikubwa cha maambukizi ya homa ya ini kwa waathirika wa dawa.

**HOSPITALI MIREMBE**

Mkurugenzi wa Hospitali ya Mirembe na Kituo cha Itega, Dk. Erasmus Mndeme, katika taarifa yake anasema waraibu wanawafikia kupitia asasi zisizo za serikali.

Dk. Mndeme anabainisha, kwa sasa kituo kina waraibu 479 na kati yao 367 wanatumia dawa aina ya methadone kila siku.

Pia, katika kundi hilo kuna waraibu 26 wanaoishi na virusi vya ukimwi(VVU) na kati yao, wapo wanne waliogundulika kuumwa maradhi ya kifua kikuu.

"Wengine 176 walipimwa homa ya ini, ambao 64 sawa na asilimia 36, waligundulika kuwa na homa ya ini aina ya 'B' na C," anasema.

Dk. Mndeme anaiomba kamati iwe balozi wa upatikanaji ajira na ushirikishwaji waraibu katika shughuli za kijamii, ili wajiongezee kipato.

**NGO& MRAIBU**

Meneja wa asasi isiyo ya kiserikali inayopambana na dawa za kulevya (Mefada), Alex Chitawala, anasema kuanzishwa kituo cha Itega, kimeondoa kwenye mzunguko kiasi cha Sh. bilioni 2.7 zilizokuwa zikitumiwa na waraibu 367 kila mwaka, kununua dawa ya kulevya aina ya heroin.

Anasema, asasi zisizo za serikali zina mchango mkubwa katika kupambana na dawa za kulevya na wamekuwa wakiwafuata 'vijiweni' kuwaengua kutoka matumizi ya sumu hiyo kwa maisha yao.

Chitawala anakiri vita vikubwa, kwa sababu wameondoa fedha kwa wauzaji na anafafanua mchanganuo ulivyo: "Kete moja ya heroin Dodoma inauzwa Sh.7, 000 na kiwango cha chini cha matumizi kwa mtu mmoja ni kete tatu kwa siku.

AFYA

BAADA MIAKA 11...

# Simulizi za mwanasheria William ukomo mauaji ya wenye ualbino

• Toka zama za kulia, hadi kicheko • Ubia wao na Under the Same Sun



Watoto wenye ualbino wakiwa katika mikusanyiko tofauti, yenye huduma na harakati za kupigania haki zao. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Romana Mallya**

NI kicheko. Ndivyo unavyosema baada ya kundi la watu wenye ualbino ambalo miaka 11 iliyopita, aliliishi kwa shaka na hofu kubwa ya kuuawa au kukatwa sehemu ya miili yao. Sasa wanatembea kifua mbele, kutokana na vitendo hivyo kudhibitiwa kwa kiasi kikubwa.

Maduhu William ni miongoni mwa watu wenye ulemavu wa ngozi, ambaye kitaaluma ni mwanasheria na anathibitisha kuwapo usalama kwa sasa.

"Tulikuwa tunaishi kwa hofu na mashaka, tukihofia usalama wa maisha yetu. Fikra zetu ziliona kila anayekuja mbele yetu ni mhalifu kwetu, anataka viungo vyetu au uhai wetu.

"Kwa sasa maisha yamebadilika tupo kwenye usalama, tunapata elimu na tunatumia taaluma zetu kuwasaidia wengine," William ndivyo anavyoanza kueleza

William, Mwanasheria wa shirika la Under the Same Sun (UTSS), aliyezungumza na Nipashe kuhusu kuanzishwa kwa shirika hilo, hafichi tabasamu lake kubwa ni kiashiria cha amani iliyopo kwa kundi hilo, baada ya kupita zama za vitishio kwao.

Ni mazungumzo yaliyochukua dakika 60, kati yake dakika 40 zinatawaliwa na simulizi ya mafanikio.

Kila siku ya Februari 24, asasi ya Under The Same Sun hufanya maadhimisho ya kumbukumbu hiyo, ambayo katika hadhira ya mwaka huu, mtaaluma wao wa sheria, William anakiri wasiwasi na vitisho dhidi yao vimepungua sana, kundi lao likifurahia mafanikio, ambayo pia yaliacha simanzi kutokana madhara yake.

> **Kabla ya kutumia dawa, lazima ujue hivi vimelea vina shambulia sehemu gani ya mwili wako. Baada ya hapo daktari anaweza kukushauri utumie dozi ipi, tiba ipi na kwa dozi ya kiasi gani.**

William anaanza kueleza kuwa, shirika hilo lilianzishwa kwa madhumuni makubwa mawili anayoyataja:"Kutoa elimu kwa Watanzania kujua kwa nini mtu anazaliwa na ualbino na changamoto zake."

Pili, anasema shirika hilo lilianzishwa ili kutoa ufadhili wa elimu kwa jamii hiyo katika ngazi mbalimbali, kuanzia awali hadi chuo kikuu.

Anasema, hadi sasa tangu kuanzishwa kwake, wanufaika wa elimu wamefikia 420 na miongoni mwao, wapo wahitimu ambao sasa wanafanya kazi katika maeneo tofauti ikiwamo serikalini.

### SAFARI WALIKOTOKA

William anasema maadhimisho ya mwaka huu yamelenga kuangalia safari yao walikotoka, walipo na wanakoelekea.

"Tulikotoka ni mbali, hali ilikuwa tete. Ukiangalia usalama wa hili kundi hali ilikuwa mbaya kwelikweli, watu walikuwa wanauawa, wanakatwa mkono au mikono au viungo vingine mwilini.

"Miaka ya 2008 na 2009, hadi mwaka 2015 usalama wetu ulikuwa shakani. Waliokuwa shule walikuwa wachache, kutokana na uelewa wa wananchi na walimu. Hii ilichangia hata ajira kwetu zilikuwa changamoto, waajiri wengi walikuwa na uelewa mdogo, hawakutuona kama tunaweza."

William anataja eneo lingine lililokuwa na changamoto, ni uelewa mdogo wa wananchi, unyanyapaa uliokuwa katika kiwango cha juu, ukimbatana na lugha za kejeli.

Mwanasheria huyo anakumbusha kuwa changamoto hizo ndizo zilizosababisha kuanzishwa shirika hilo la UTSS, ambalo mwasisi wake ni Peter Ash, raia kutoka Canada.

Anasema, eneo lingine lililokabiliwa na changamoto ni ngozi zao, ambazo wenye ualbino walikuwa na uelewa mdogo wa kuzitunza, hivyo ikasababisha wengi wao kupata maradhi ya saratani.

"Walikuwa hawajui kama wanatakiwa kuvaa kofia pana, kuvaa mavazi yanayoficha ngozi, kupaka losheni maalum ya ngozi. Wengi walipoteza maisha kwa sababu ya saratani ya ngozi.

"Ilikuwa ukitembelea hospitali ya Ocean Road, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MHN), Hospitali ya KCMC, utakuta wagonjwa wengi wamelazwa kwa sababu ya jua lililosababisha ngozi kupata saratani."

### WALIKOFIKIA

William anasema, kwa kiwango kikubwa wengi wao wamepata elimu na kuelimika na sasa wanamjua mtu mwenye ualbino ni nani, hivyo imefuta fikra potofu dhidi yao hata baadhi kushiriki kuwaua.

"Utaona sasa mauaji yamepungua sana. Yalikuwa yakitokea kwa sababu watu wengi walikuwa na uelewa mdogo. Watu wamefahamu sisi ni binadamu wenzao, tofauti iliyopo ni rangi tu.

"Leo, ukizungumzia usalama wetu upo wa juu sana, hofu inapungua siku hadi siku, tunafanya shughuli zetu vizuri usiku na mchana.

"Eneo la pili ambalo linaashiria kwamba uelewa umekuwa mkubwa ni ajira, tunaona kwa sasa tuna viongozi wa taifa, tuna balozi mwenye ualbino, tuna naibu katibu mkuu, wabunge. Yote ni kiashiria kwamba uelewa umekuwa mkubwa," anasema.

Mwanasheria huyo anataja eneo la tatu, ni kwamba katika miaka ya nyuma walikuwa wakipokea kesi nyingi za wazazi kutekeleza watoto wenye ualbino, akiifafanua kwa kauli:

"Ilikuwa ukizaa mtoto mwenye ualbino, haikuwa furaha kwa mama, kwa sababu mzazi mwenzake wa kiume alikuwa akitelekeza familia na kuikimbia.

"Mama naye akiona amekimbiwa, alikuwa akimchukua mtoto na kumpeleka kijijini kwa babu au bibi kwa kuogopa kuchekwa. Hii ilisababisha takiwmu za watu wenye ualbino nyingi kuonyesha, malezi yao ni ya upande mmoja, yaani mama au babu au bibi.

"Leo tunapokea simu za pongezi wazazi wanauelewa wanakuja kwenye ofisi za shirika hili zilizopo Mikocheni jijini Dar es Salaam, kueleza kuwa wamezaa mtoto mwenye ualbino wanataka elimu namna ya kuwalea.

"Tunawapa elimu, baba wa mtoto anaahidi kuwa 'huyu ni mwanangu nitamlea kwa gharama zote na nitamlinda kwa gharama yoyote' yote hii inaashiria kuwa uelewa umeongezeka sasa."

William anasema kesi za watoto kutelekezwa ambazo hapo nyumba zilikuwa nyingi, lakini kwa sasa zimepungua.

AFYA

# Simulizi za mwanasheria William ukomo mauaji ya wenye ualbino



Watoto wenye ualbino wakiwa katika harakati za kupigania haki zao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Kingine, miaka ya nyuma tulikuwa na watoto wengi waliokuwa wanaishi vituo maalum vya kulelea watoto, leo ukienda namba yao imepungua sana. Ilifikia hatua vituo vilizidiwa idadi ya watoto ilikuwa kubwa kati ya 200 hadi 300.

"Kwa sasa wanarudi makwao wanajumuika na familia zao, kwa sababu tu usalama upo na wanatembea usiku na mchana bila ya kupata tatizo. Uelewa wa wananchi kwa sasa tumefikia asilimia 70," anaeleza bila ya kuzifafanua hizo asilimia kwa kina.

Kwenye elimu, anasema kwa sasa wengi wao ni wasomi wamekanyaga ngazi ya vyuo vikuu na kutunukiwa shahada za kwanza, baadhi za pili na wapo waliokwea hadi kuwa na shahada za uzamivu, hadi udaktari falsafa.

William anasifu elimu ya kundi lake limewakweza kupata ajira bora na wapo walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali serikalini na katika taasisi mbalimbali za umma.

**KUELEKEA UCHAGUZI**

William anasema shirika lao kwa sasa, linaendelea kutoa elimu na katika mazungumzo yake na Nipashe anasema kwamba, baadhi ya wafanyakazi walitoka mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kueneza uelewa huo.

"Hatuwezi kuacha kutoa elimu, tutaendelea ili kila mmoja wetu atambue kuwa mtu mwenye ualbino anastahili kuishi.

Pia, anatoa wito kwa wadau wa uchaguzi na vyama vya siasa kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa Oktoba ijayo, mtu kutoka kundi hilo anapoonyesha nia ya kugombea, daima apewe ushirikiano.

"Ikitokea mwenye ualbino amechukua fomu kugombea nafasi ya kisiasa apewe ushirikiano kama mwananchi mwingine kwa mujibu wa ibara ya tano ya Katiba inayotoa haki ya mtu kuchagua na kuchaguliwa.

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi, iweke mwongozo na kanuni ambazo zitasaidia wagombea walemavu wakiwamo wenye ualbino, walindwe kwa sababu ipo tabia ya wagombea wakati wa kujinadi wanatoa lugha za kejeli au kashfa, matusi au kumaanisha mtu ulemavu aliyo nao," anasema.

William anaeleza ushuhuda kutoka Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, katika mkoa wa Kusini mwa nchi mwenye ualbino kukejeliwa kuhusiana na ulemavu wake na anayefanya hivyo, ni mshindani wake katika ulingo wa kisiasa.

William anatoa angalizo, akisema katika miaka ya nyuma walishuhudia matukio ya kuuawa na kujeruhiwa wenye ulemavu na anongeza:

"Tunaamini uchaguzi huu utaisha bila ya kusikia tukio lolote la mtu mwenye ualbino kuzuriwa ama kuuawa. Tunajua uelewa upo wa hali ya juu na wananchi tayari wameelimika," anasema.

> "Wanachukua mabaki ya viungo vyao na kwenda navyo kusikojulikana, tunaomba vyombo husika viwachukulie hatua wahusika wote pindi wanapokamatwa.

**WAFUKUA MAKABURI**

Anaeleza elimu inayoendelea kutolewa kwenye jamii, imewezesha kupunguza matukio ya uhalifu kwa wenye ulemavu wa ngozi, lakini kunaibuka sura nyingine ya kuwepo changamoto kwa baadhi ya wahalifu ambao sasa wamebadili mbinu, kukimbilia makaburini kufukua miili ya wenye ulemavu wa ngozi.

"Wahalifu badala ya kutuua au kutujeruhi, wamebadilisha mbinu wakihofia mkono wa dola, hivi karibuni huko Mbeya na Njombe kumejitokeza matukio ya kufukuliwa makaburi ya zamani ya ndugu zetu waliozikwa.

"Wanachukua mabaki ya viungo vyao na kwenda navyo kusikojulikana, tunaomba vyombo husika viwachukulie hatua wahusika wote pindi wanapokamatwa," anaomba.

William, katika nafasi ya pekee anamshukuru Rais Dk. John Magufuli na serikali yake kuwa mstari wa mbele kuhakikisha hakutokei matukio ya kuuawa ama kujeruhiwa.

Anasema elimu inayoendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali, imewezesha wazazi wenye watoto walio na ualbino kwenda katika shirika hilo kupata elimu namna ya kuwalea ili wasipate saratani ya ngozi.

"Kwa mwaka huu hadi sasa jumla ya familia sita zimejitokeza na mwaka jana zilikuwa zaidi ya 30, wanakuja kuomba ushauri wa malezi ya watoto wao na wengi wanataka kujua matumizi ya losheni, ili kuzuia mionzi ya jua," anasema.



Maduhu William, Mwanasheria wa asasi ya Under The Same Sun. **PICHA: ROMANA MALLYA**

Hata hivyo, William anaiomba serikali kuharakisha kesi za wenzao zilizopo mahakamani, ambao walipatwa na majanga ya kuuawa au kujeruhiwa kuanzia mwaka 2008

**MADHILA YALIVYOKUWA**

Ni madhila yanayokinzana sana na haki za binadamu. Kuna matukio kadhaa ya vifo na kujeruhiwa kwa watoto wadogo yalishamiri katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, huku yakihusishwa na imani za kishirikina na utajiri.

Baadhi ya wazazi walijitoa ufahamu na kugeuka wahalifu kwa kushiriki mauaji ya watoto wao, ili watajirike, kitendo ambacho siyo kweli.

Uchimbaji madini, siasa na imani za waganga wa kienyeji, zilitajwa kuwa vishawishi vikuu vya kutaka viungo vya watu hao, ili mambo yao yanyooke.

Juhudi za kudhibiti matukio hayo zilifanywa na serikali kupitia Jeshi la Polisim ndiyo inamfanya William badala ya kueleza changamoto, anasimulia hatia ya ukombozi kwa furaha, kutokana na juhudi zilizofanywa kukabiliana na tatizo hilo.

AFYA

# Staili 'namba mbili' kukabili hodi ya corona barani Afrika



Kujihami na corona nchini Nigeria. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

BAADA ya Nigeria kutangaza tukio la kwanza la homa ya corona kutoka kwa mtu anayesadikika alitokea nchini Italia. Nchi nyingine kadhaa za Afrika, ziko katika uwezekano wa matukio kama hayo.

Hatari ni endapo ataingia mtu nchini, akiwa bado virusi vya corona (au inavyoitwa corona mpya, COVID-19) havijachangamka mwilini kuanza kupandisha joto, hivyo havionekani kirahisi. Inakuwa mwanzo wa kuenea ugonjwa huo.

Kipindi kati ya kuambukizwa na dalili kuonekana ni kigumu, kwani wataalamu wanasema vipimo wakati huo huenda havionyeshi chochote. Kimsingi, mtu huyo anaweza akaruhusiwa aende.

Jinsi maambukizi yalivyohamia nchi nyingine, inaelekea homa ya corona inaambukiza kwa kasi kuliko magonjwa mengine na kwa kiasi fulani, inafanana na ebola.

Barani Afrika, madhara yake hayajasambaa katika eneo kubwa, lakini kwa watu wanaowakaribia sana walioambukizwa, uwezekano wa kupata ugonjwa huo unakuwa mkubwa.

Corona imeshaua madaktari na manesi katika hospitali ya jiji la Wuhan huko China, ambako mlipuko ulianza; waliambukizwa kabla tahadhari haijaanza.

Katika nchi tofauti, kuna mijadala ya kisiasa na kitaaluma iliyokwishaanza au imepamba moto, ni jinsi gani nchi husika zimejiandaa kwa janga la homa ya corona, nini cha kufanya kuzuia kuenea kwake na hata kuua watu wengi.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani na mengine (ikiwamo Taasisi ya Magonjwa ya Tropiki ya Ufaransa), nchi za Afrika zina viwango tofauti vya uwezekano wa maambukizi, kutokana na wingi wa safari za ndege kwenda au kurudi kutoka China.

> Kila mahali zikiwepo hizo halafu zisaidiane na zile za kutibu ugonjwa husika (yaani mafua na homa kali, zaidi 'antibiotics'), kinga inaweza kujengwa.



Ukaguzi dhidi ya corona nchini Algeria.

Pia, nchi hizo zina tofauti za uwezo wa kukabili ugonjwa huo, iwapo itazingilia na kuwapo mtu aliyeambukizwa, ambaye hajagundulika anapoingia nchini.

Corona inaelezwa, inajidhihirisha tofauti kati ya nchi moja na nyingine katika kugundua maambukizi yake, kujua yalikotokea na kuwazuia majumbani waliokutana na vyanzo hivyo vya maambukizi.

Taarifa zinazopatikana kutoka Uingereza na Marekani, zinaonyesha uwezo wa hali ya juu wa kufuatilia 'nyendo za corona,' hali ambayo si rahisi katika nchi za Afrika, hivyo kuwapo hatari kubwa ya kasi ya maambukizi.

Nigeria ilitangaza tukio moja la maambukizi na likapita, bila kuwapo mshituko zaidi. Nchi zilizopata matatizo makubwa zaidi na homa ya corona, ni ambazo maambukizi ya awali yalitokea katika hadhara fulani, mfano katika masoko ya nyama maalum kabla ya sikukuu mwaka mpya wa Kichina.

Pia, nchini Korea Kusini, ilikuwa katika hadhara ya kidini, hivyo waanza kufuatilia wote waliokuwapo na kuwazuia wasitoke. Ilikuwa kazi ngumu sana.

Maambukizi ya nchini Uingereza na Marekani, hasa yalitokana na watu waliosafiri kwenda nchi za China, Iran na Italia wakaambukizwa huko.

Wakati taasisi za kimataifa za masuala ya afya zinaeleza jinsi Afrika ilivyo na ukaribu na China, hata wakapima uwezekano wa maambukizi kuwafikia kutokana na safari za ndege, bado haijazungumziwa kwa karibu mpangilio wa kukabiliana na hatari ya kusambaa kwa homa hiyo.

Uingereza inasema, imeandaa vitanda 300 kukabili hali, pindi ikitokea wimbi la maambukizi na itaendelea zaidi.

### AFRIKA ILIKOSIMAMA

Nchi za Afrika kwa jumla zimekuwa kimya, zikihofia kutangazwa ugonjwa huo kuingia katika nchi zao. Tahadhari zimewekwa zaidi katika viwanja vya ndege vya kimataifa.

Ndani ya nchi kwingi kuna ukimya mkuu wa matayarisho ya mapokezi ya wagonjwa au mfumo wa tiba, bila ya kuzungumzia gharama na mikakati, endapo homa itaenea.

Tatizo la msingi la mkakati kama huo, ni haraka ya maradhi kuenea katika mazingira ambako watu ni wengi katika makazi na siyo rahisi kufuatilia historia yake, kama vile watu aliyokutana nao.

Pia, kuna suala la uharaka wa tiba, ambao katika hali ya kawaida, kulaza wagonjwa hospitalini bado ni tabu. Hapo inaendana na haraka ya vipimo na kiwango cha tija katika taasisi zilizopo za kutoa huduma ya afya.

Katika sura ya pili, ikirejewa corona ni mithili ya flu au mafua makali yanayoenea kwa haraka, ni wazi kunakuwapo hitaji la mkakati wa wepesi wa kugundua na kuhudumia dalili, zikafanyiwa kazi katika hatua ya awali, hata pale mtu alipo.

Bado hakujawepo matumizi ya mitandao kama vile simu, endapo mtu anapatwa na dalili za tatizo hilo, anapatiwa ushauri wa haraka kuhusu dawa au mbinu za matibabu zinazopaswa kufuatwa, pasipo kuchelewa.

Lingine muhimu, si ajabu pia kuwepo mkakati wa msingi wa dawa za kuanzia na hasa kujenga kinga mwilini kwani uharaka wa kudhoofika unatokana na kinga kupungua kwa haraka. Hapo kuna mtihani wa 'ukuta dhidi ya corona.'

Majadiliano kuhusu homa ya corona hayajagusa tiba za haraka katika nchi tofauti, kwani kimsingi ni mafua makali na homa. Zaidi kuna utafiti wa kupata chanjo ambayo baadhi wanasema itachukua mwaka mmoja au na nusu. Ila kuna watafiti nchini Israel wakishirikiana na wenzao wa Marekani, wanasema ni wiki kadhaa tu.

Kimsingi, hatari ya kuenea kwa homa ya corona ipo na haikwepeki, kwani kupenya mtu mmoja kutoka nchi iliyoambukizwa wakati maambukizi yanaenea ni jambo gumu kuzuia. Zaidi ya hapo, kasi ya kuenea kwa homa hiyo kutokana na watu kuwa wengi hasa katika maeneo ya makazi, ni changamoto kabambe kwa mkakati wowote ule wa kukabiliana na homa hiyo nchini au kwingine barani Afrika.

Inabidi kuwapo vipengele viwili vya kujenga ukuta dhidi ya corona. Kwanza, ni upatikanaji dawa za kujenga kinga kwa haraka mwilini (hasa 'multivitamin' zilizowasaidia sana wenye virusi vya ukimwi na hata vidonda vya saratani vilivyopanuka.

Kila mahali zikiwepo hizo halafu zisaidiane na zile za kutibu ugonjwa husika (yaani mafua na homa kali, zaidi'antibiotics'), kinga inaweza kujengwa.

Aidha, kuna umuhimu wa kuwapo kwa dawa za msingi zinazofahamika kutapunguza lazima wa kupeleka wagonjwa hospitali kungoja vipimo na kuandikiwa, kwani itakuwa balaa.



# Wanufaika Tasaf kufuatiliwa kidigitali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema inaandaa mpango wa kufanya uhawilishaji wa wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) ambao unatekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini kidigitali ili kuepuka kuwa na kaya hewa na wanufaika wasiokuwa na sifa.

Aidha, inaandaa kiapo maalumu cha uadilifu ambacho maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri zote nchini ambao wanaosimamia mpango huo watakuwa wanaapa na kwamba wakikiuka kiapo hicho watakuwa wanaadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa juzi jijini Mbeya na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alipokuwa anazungumza na viongozi wa Mkoa wa Mbeya kabla ya kuanza ziara ya kukagua maendeleo ya wanufaika wa Tasaf.

Mwanjelwa alisema katika awamu zilizopita kuliibuka wimbi kubwa la wanufaika hewa na kwamba baadhi ya waliokuwa wananufaika, hawakuwa na sifa za kunufaika.

Alisema wanufaika wa mfuko huo wataunganishwa na mfumo wa GPS ambao utarahisisha ufuatiliaji na uhakiki ili kuhakikisha kila anayeingia kwenye mfuko huo ni mlengwa sahihi na hata wakati wa kufuatilia iwe rahisi kumkuta.

"Pia itaundwa timu maalumu ya ufuatiliaji wa wanufaika, watakuwa wanawatembelea wanufaika kwenye maeneo wanayoishi, wakati wataalamu hao wanapofanya kazi watapigwa picha wao pamoja na wanufaika wanaowahakiki na taarifa zitaingia moja kwa moja kwenye mfumo," alisema Mwanjelwa.

Alisema utaratibu wa mikutano ya vijiji na mitaa ambayo imekuwa ikitumika kupendekeza kaya zinazostahili kunufaika na mfuko huo itaendelea kufanyika na mfumo wa digitali ni kwa ajili ya uhakiki.

Alisisitiza watahakikisha wanaondoa matatizo yote ambayo yalibainika kwenye awamu zilizopita za mfuko huo ambazo hivi karibuni, Rais John Magufuli, aliziainisha kwenye hotuba yake wakati anauzindua upya mfuko huo.

Mratibu wa Tasaf wa Mkoa wa Mbeya, Haika Temu, alisema kuanzia mwaka 2015 mpaka sasa zaidi ya Sh. bilioni 42 zilipokelewa na kugawanywa kwa walengwa wa mfuko huo katika halmashauri zote za mkoa huo.

Alisema ofisi yake kwa kushirikiana na maofisa maendeleo wa wilaya na viongozi wengine wamekuwa wakifuatilia maendeleo ya kaya zinazonufaika na kwamba kuna mabadiliko makubwa ya kimaisha.

Temu alisema kutokana na mfuko huo, baadhi ya wanufaika wameboresha makazi na kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kilimo, ufugaji, ususi na biashara ndogo ndogo hali ambayo inawapa uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku.

Vilevile alisema kumekuwa na ongezeko la mahudhurio ya watoto wanaotoka kwenye kaya maskini kwenye huduma za jamii ikiwamo shuleni na kliniki.

"Tatizo lililopo ni kwamba baadhi ya wanufaika wamekuwa wakizitumia fedha hizo kwa matumizi yasiyofaa ikiwamo kunywea pombe na kuhonga, lakini baadhi ya mitaa haijawahi kunufaika na mfuko huu tangu ulipoanza na ina watu wenye sifa," alisema Temu.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa (wa pili kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (kulia), wakinengua pamoja na baadhi ya wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wa Mtaa wa Pambogo Kata ya Iyela, jijini Mbeya juzi, katika ziara ya kuwatembelea wanufaika hao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Itende sasa walilia ukarabati barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Itende katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameiomba serikali kukarabati barabara inayoanzia katika njia panda ya Itende kwenda mpaka Mtaa wa Mkuyuni ili kuwarahisishia usafiri.

Waliyasema hayo juzi wakati wa ziara na Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, ambaye alitembelea kata hiyo kwa ajili ya kuwasilisha msaada wa mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Msingi Mkuyuni.

Wananchi hao walisema usafiri wanaoutumia kwenye eneo hilo ni bajaji na pikipiki na kwamba usafiri wa gari ni shida kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu na yenye mashimo na matope ambayo yanasababisha magari kukwama.

Zakayo Ndele, alisema kutokana na mvua inayoendelea kunyesha kwa sasa hata bajaji zinashindwa kufika mpaka mwisho, hivyo wanalazimika kutembea kwa mguu mpaka kuzifikia zinapoishia.

"Mvua ikinyesha unaweza ukadhani huu ni mto kumbe ni barabara, maji yote yanayotoka kwenye mitaa ya juu yanakusanyika na kupita humu kwa hiyo inakuwa ni shida kubwa, tunaomba serikali itusaidie," alisema Ndele.

Akizungumzia tatizo hilo Dk. Tulia alisema yeye na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, watawasilisha kilio hicho kwenye mamlaka zinazohusika ili irekebishwe.

Alisema lengo lake kwenda katika eneo hilo ilikuwa ni kuwasilisha mchango wake kama alivyokuwa ameombwa na uongozi wa shule hiyo na kwamba hata yeye alionja adha ya ubovu wa barabara hiyo.

"Ni kweli hili ni tatizo kwa hiyo tunalichukua na tutalifikisha kwa wahusika kwa ajili ya utekelezaji na hata matatizo mengine mliyoyasema hapa tunayachukuwa na yatafanyiwa kazi," alisema Dk. Tulia.

# Ziwa Rukwa, Nyasa hatarini kupotea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZIWA Rukwa na Ziwa Nyasa ambayo yapo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, yapo hatarini kukauka kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kwenye vyanzo vya maji ya mito inayomwaga maji kwenye maziwa hayo.

Hayo yalisema na wasimamizi wa mabonde hayo kwenye mkutano wa pamoja wa mabonde matatu ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa na Bonde la Mto Rufiji kujadili utekelezaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasirimiali maji kwenye mabonde hayo.

Ofisa wa Maji wa Bonde la Ziwa Rukwa, Grace Chitanda, alisema bonde hilo linakabiliwa na mabadiliko makubwa ya tabianchi yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu kikiwamo kilimo na ufugaji ambazo zimekuwa zikifanyika kwenye mito.

Alisema kutokana na shughuli hizo, baadhi ya mito inayomwaga maji kwenye ziwa hilo imeanza kukauka ukiwamo Mto Katuma na kwamba kwenye baadhi ya mito maji yamepungua ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Alisema wanakabiliana na tatizo hilo kwa kushirikiana na taasisi zingine ikiwamo maofisa wa Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi za Taifa (Tanapa) kuzuia shughuli zozote kwenye vyanzo vya mito.

"Wakulima wa mpunga wamekuwa wakianzisha mifereji mingi ya kienyeji kwenye mito na hivyo kuharibu mtiririko wa maji, Mto Katuma ulikuwa na mifereji 48, lakini t umeshirikiana na wadau kuifukia mpaka imebakia nane pekee," alisema Chitanda.

Alisema bonde hilo pia lina idadi kubwa ya mifugo ambayo imekuwa ikichungwa na kunyweshwa maji kwenye mito na hivyo kusababisha kiwango cha maji kupungua kwa kiasi kikubwa.

Alisema ili kukabiliana na janga hilo wamependekeza serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira kujenga mabwawa ya kuvunia maji ya mvua ambayo yatatumika kunyweshea mifugo na kutumika kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Naye Mwenyekiti wa Bonde la Ziwa Nyasa, Mhandisi Ngwisa Mpembe, alisema wanaendelea na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji ili kuwa na rasilimali endelevu za maji.

Alisema katika maeneo mengi ya vyanzo vya maji ya Ziwa Nyasa, baadhi ya wananchi wamekuwa wakikata miti na kusababisha maji kupungua kwenye mito na hivyo kuhatarisha uwepo wa Ziwa hilo miaka ijayo.

Alisema ziwa hilo linashirikisha mikoa minne ya Mbeya, Njombe, Songwe na Ruvuma, hivyo kwa sasa wanashirikiana na wadau mbalimbali kukabiliana na matatizo yaliyopo.

Mkurugenzi wa Rasilimali Maji kutoka katika Wizara ya Maji, Dk. George Lugomela, alisema mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa raslimali maji iliandaliwa mwaka 2015 na ilikuwa inaendelea kutekelezwa katika kipindi chote cha miaka mitano.

Alisema mpango huo ulikuwa umegawanyika katika awamu tatu ambazo ni mpango wa muda mfupi ambao ni miaka mitano kufikia 2020, muda wa kati ambao ni miaka 10 mpaka kufikia 2025 na muda mrefu ambao ni miaka 30 mpaka kufikia 2035.



# Wagombea uenyekiti CCM Dodoma waonywa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAGOMBEA wa nafasi ya uenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Dodoma wameonywa kujiepusha na vitendo vya rushwa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Machi 7, mwaka huu.

Uchaguzi huo unatokana na Mwenyekiti aliyekuwapo Robert Mwinje, kuondolewa kutokana na matumizi mabaya ya madaraka Desemba 18, mwaka jana.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, Elirehema Nassari, Nassari alisema katika kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, Februari 28, mwaka huu, kiliteua majina ya wagombea watatu ambao watawania nafasi hiyo.

"Wagombea walioteuliwa ni pamoja na Dk. David Malole, Vanesa Malika na Johanic Salingo, hawa ndio watasimama kuwania nafasi hiyo na uchaguzi utafanyika Machi 7, mwaka huu na wapigakura watakuwa 1,300," alisema.

Aliwataka wanachama na viongozi kuachana na vitendo vya rushwa ili kuchagua kiongozi ambaye hatokani na rushwa.

"Kama ambavyo Mwenyekiti wa chama amekuwa akijipambanua ni mtu asiyependa rushwa niwaombe sana na niwasihi wawe makini na vitendo vyovyote ambavyo vitaashiria kwamba kuna mazingira ya rushwa," alisisitiza.

Aliwataka wagombea kuomba kura kwa ustaarabu na kuwaeleza wanachama watawafanyia nini katika kipindi cha miaka miwili iliyobaki kuanzia mwaka 2020 hadi 2022.

"Kwa hiyo nitoe rai viongozi wangu, wagombea wangu tafadhali sana msijihusishe na masuala ya rushwa lakini kubwa kuliko yote tufanye kampeni za kistaarabu, jambo lingine niwaombe viongozi wangu wasiahidi mambo ambayo yapo kinyume na kanuni na taratibu zetu," alisisitiza.

Kuhusu kuondolewa kwa Mwinje, Katibu huyo alisema aliondolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 18(I) ya chama hicho.

"Kanuni inasema ataondolewa kwa kutumia vibaya madaraka aliyopewa ama kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ile ni kinyume na lengo lililokusudiwa," alisema.

"Ndugu yetu mwenyekiti alitumia vibaya madaraka yake ya uenyekiti ndio sababu kubwa ambayo imemwondoa kwenye nafasi hiyo, baada ya kuondolewa tulianza mchakato wa kutafuta mwenyekiti mpya."

Alifafanua kuwa katika mchakato huo, wanachama 38 walijitokeza kuchukua fomu na utaratibu wa uchujaji wagombea ulianza na hatimaye wamebaki watatu.

"Kwa mujibu wa kanuni yetu Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM, Wilaya ya Dodoma Mjini ndio kikao cha kwanza kinachoanza taratibu nzima ya uchujaji, kamati ya siasa ilikaa ikapendekeza kwa kamati ya siasa ya mkoa na kamati ya siasa ya mkoa ndio ikapendekeza kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa," alisema.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa (kushoto), Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), Justina Mashimba (katikati) na Mkurungenzi Mtendaji wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Hisham Hendi, wakibonyeza kitufe cha kompyuta jijini Dodoma jana, kuashiria uzinduzi rasmi wa mradi wa kuunganisha shule 163 kwa mtandao wa intaneti, ambapo Vodacom imetoa kompyuta 806 pamoja na vifaa kiungaishi mfumo wa intaneti (router), kwa ajili ya shule hizo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yakomalia vibali vya mchele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuzuia vibali vya kuagiza nje ya nchi mazao ya chakula yanayozalishwa kwa wingi nchini ikiwamo mchele.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe katika mkutano wa Baraza la Mchele Tanzania ambao ulikuwa ukijadili uzalishaji bora na endelevu ili kuongeza tija kwa wakulima wa zao hilo.

Alisema serikali itaendelea kusimamia uagizaji wa mchele kutoka nje ya nchi na ndio msimamo wa serikali.

"Huu ndio msimamo wa serikali kwamba hatuwezi kuruhusu muagize mazao ya chakula ambayo sisi wenyewe tunazalisha kwa wingi, tunazalisha tani milioni moja za mpunga lazima tujiwekee malengo ili kuwa na uzalishaji wa tani milioni tatu hadi nne," alisema.

Bashe alisema lengo ni kukidhi mahitaji ya nchi.

"Baada ya mkutano huu nitaomba nipate ripoti ambayo itaonyesha malengo tuliyojiwekea, na namna gani tutaboresha uzalishaji wetu ili kuzalisha tani milioni tano kwa mwaka za mchele, na uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwenye mchele na tutaongezaje uzalishaji wa mbegu za mpunga," alisema.

Pia alisema kama serikali walenge kwenye uzalishaji wa mbegu ya aina wanayoipenda.

"Lazima tuwe na mchele unaowiana na mazingira yetu na uasili wetu kama vile Super," alisema.

Nao baadhi ya wadau kwenye mkutano huo, walisema kuna tatizo la vifungashio na kuhamasisha wakulima kuachana na matumizi ya vifungashio visivyo na ubora ili kupunguza upotevu wa mazao.

# Huduma shikizi tiba methadone kuanzishwa Dar es Salaam

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuanzisha huduma shikizi za tiba ya methadone kwa waathirika wa dawa za kulevya aina ya heroin kwenye Jiji la Dar es Salaam kutokana na kuwapo na msongamano mkubwa wa wagonjwa hao.

Hayo yalielezwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Mirembe na Kituo cha Methadone cha Itega, Dk. Erasmus Mndeme, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya huduma za methadone pamoja kituo hicho kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi na Dawa za Kulevya.

Alisema kuna msongamano mkubwa katika maeneo yanayotoa huduma za methadone kwenye jiji la Dar es Salaam na kwa sasa kwenye kliniki zote tatu zilizopo idadi ya wagonjwa ni maradufu ya makadirio ya awali.

Alisema hadi kufikia Januari 2020, wagonjwa 7,658 wanapata huduma ya methadone kati yao 6,682 sawa na asilimia 87 wapo kwenye jiji hilo.

"Awali ilikadiriwa kuwa na wagonjwa kati ya 1,000 hadi 1,500 kwa kituo, lakini hali hii inasababisha waratibu wa huduma hizo katika ngazi ya Taifa na kupitia vikao vya pamoja vya waratibu na watoa huduma kufikiria mbinu mbadala ya kuboresha huduma hizi kwenye vituo vyetu," alisema.

Alisema mojawapo ya mbinu zilizokubalika ili kukabiliana na hali hiyo ni uanzishwaji wa 'satellite' kliniki nne kwenye vituo vilivyopo katika ngazi za halmashauri na kituo kimoja kwenye Gereza la Segerea ifikapo Desemba 2020.

Dk. Mndeme alisema mkakati huo utapunguza msongamano kwenye kliniki hizo na hivyo kutoa mwanya kwa watoa huduma kuwa na muda zaidi wa kuwaona wagonjwa na kuwapa huduma stahiki.

"Pia kupeleka huduma kwenye halmashauri karibu na makazi ya waathirika ili kuwapunguzia gharama za usafiri na uhatarishi wa kupata magonjwa ya kuambukiza ambayo kwa bahati mbaya kundi hili limekuwa na changamoto kubwa ya maambukizi ya magonjwa ikiwamo, kifua kikuu, homa ya ini na VVU/Ukimwi," alisema.

Awali, Mkurugenzi huyo alisema huduma za methadone nchini zimeongezeka tangu zilipoanzishwa mwaka 2011 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

"Hadi kufikia Januari 2020, jumla ya wagonjwa 7,658 wanapata huduma ya methadone kati yao wanawake ni 471 sawa na asilimia 6.2 na wagonjwa 6,682 sawa na asilimia 87 wanapata huduma jijini Dar es Salaam," alisema.



## Gavana BoT ateta na Rais wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imefurahishwa na taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliyoitoa ya kuendelea kukua kwa uchumi wa Zanzibar.

Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na Gavana wa Benki Kuu, Profesa Florens Luoga ambaye alimweleza Dk. Shein jinsi uchumi wa Zanzibar unavyoendelea kuimarika.

Dk. Shein kwa upande wake alisema kuwa hiyo ni habari njema ambayo inatoa mwanga wa maendeleo ya uchumi wa Zanzibar na juhudi za makusudi bado zinaendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha uchumi unaimarika zaidi.

Rais Dk. Shein alisema hatua hiyo imefikiwa kutokana na uwapo wa uongozi bora na ushirikiano mzuri kati ya serikali, wananchi na Benki Kuu.

Alisema katika suala la mfumuko wa bei pia, amepokea kwa furaha maelezo ya kuwa mfumuko wa bei uko vizuri hali ambayo inaleta faraja kwa wananchi.

Alisema Zanzibar haina shida ya chakula na wananchi wamekuwa wakila chakula wanachokitaka.

Hata hivyo, alieleza kuwa Serikali Zanzibar itaendelea kushirikiana na BoT hasa ikizingatiwa kwamba hiyo ni benki ya wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dk. Shein alimpongeza Gavana huyo kwa juhudi anazozichukua katika kuhakikisha benki hiyo inaimarika na inaendelea kuwa tegemeo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naye Gavana Luoga alisema uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika kila siku na kumpongeza Rais Dk. Shein kwa kuendelea kuisimamia hali hiyo.

Alisema BoT, itaendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali ya Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unazidi kuimarika kutoka wastani wa asilimia saba hivi sasa.

Pia alisema BoT haijachapisha wala kuingiza fedha mpya kwenye mzunguko tangu mwaka 2009 na kwamba iliyopo kwenye mzunguko inatosha kwa mahitaji ya soko.

Alisema BoT inaendelea na mapambano kwa watengenezaji, wasambazaji na watumiaji wa noti bandia na kueleza hatua inazozichukua katika kutoa elimu kwa wananchi ya kufanya utambuzi wa noti bandia ili kuepuka utapeli.

Alisema Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera yake ya sarafu safi huku akiziomba benki zote kuhakikisha zinatoa huduma rafiki kwa wananchi ili waweze kutumia vyema huduma hizo.

# Shein ataka uwazi usajili mali, madeni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema viongozi wote wa serikali wana wajibu wa kusajili taarifa za mali na madeni kwa uwazi, ikiwa ni hatua muhimu katika kukamilisha dhana ya utawala bora.

Dk. Shein alisema hayo Ikulu Zanzibar, wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2019/2020.

Alisema ni wajibu wa viongozi wote nchini kuweka taarifa zao kwa usahihi na uwazi wa mali na madeni waliyonayo na hakuna sababu ya viongozi kuficha.

Dk. Shein alitupongeza uongozi wa Tume ya Maadili na Viongozi wa Umma kwa kutambua dhima kubwa iliyokabidhiwa na Taifa na kutekeleza vyema majukumu yao, ambayo yanawahusisha viongozi wote wa umma.

Aliipongeza tume hiyo kwa kufanya kazi zake kuambatana na misingi ya haki na demokrasia na kutoa fursa ya kujieleza kwa viongozi wanaotuhumiwa.

Alisema ana matumaini makubwa ofisi hiyo itapata mafanikio makubwa katika siku za usoni kutokana na kasi kubwa ya utendaji kazi inayochukuliwa na watendaji wake.

Katika hatua nyingine, Dk. Shein aliutaka uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar (IPA), kuendelea kutekeleza malengo ya utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma na wananchi mbalimbali ili kuwajengea uwezo na kuliwezesha taifa kuwa na wigo mpana wa wataalamu.

Alipongeza juhudi zinazofanywa na uongozi wa chuo hicho katika utoaji wa taaluma kupitia viwango tofauti vya elimu.

Naye, Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, alipongeza uongozi wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa juhudi kubwa wanazoendelea kuchukua katika kusimamia na kupanga vyema maslahi na stahiki mbalimbali za watumishi wa umma, hatua iliyowezesha kuleta utulivu mkubwa.

Alishauri ofisi hiyo kuharakisha utoaji wa matokeo kwa wananchi na wanavyuo wanaofanya usaili wa nafasi mbalimbali za kazi, akibainisha kuwapo kwa utaratibu unaochukuwa muda mrefu hivi sasa hadi kukamilisha mchakato wa ajira kwa watumishi wapya. Alisema baadhi ya nyakati hali hiyo inaipotezea serikali watumishi wenye sifa na viwango bora vya elimu baada ya wananchi hao kuchukuliwa na taasisi nyingine binafsi au kujiunga na taasisi za Tanzania Bara kutokana na ucheleweshaji huo. Pia Dk. Abdulhamid aliushauri uongozi wa ofisi hiyo kuzingatia kwa kina changamoto ya kuwapo kwa makundi ya watumishi kutoka baadhi ya idara na taasisi za serikali wanaokwenda mafunzoni na baadaye kubadili kada, jambo alilosema linaathiri idara na taasisi wanazotoka.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji ya mpango kazi ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa niaba ya waziri wa wizara hiyo, Waziri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Gavu, alisema wizara imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mpango huo kupitia programu mbalimbali.

Alisema mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na upatikanaji wa Sh. 6,587,048,945 ikiwa sawa na asilimia 93 ya fedha zilizokadiriwa kutumika katika kipindi hicho.

Alisema miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuandaa miongozo ya usimamizi wa Tehama katika taasisi ya udhibiti wa viwango na kutoa ushauri wa kitaalamu katika uanzishaji wa mfumo wa elektroniki katika shughuli za uendeshaji na utoaji wa mizigo bandarini.




Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko (wa pili kulia), akimsikiliza Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar, Khalfan Sheikh Saleh, alipotembelea wakala huo, Maruhubi, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: OWM**

# Ukosefu takwimu wakwamisha kesi za udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya kazi kubwa zinazofanywa na waandishi wa habari katika kuripoti matukio ya udhalilishaji wa wanawake na watoto, kunakosekana kwa takwimu sahihi za matukio hayo kutoka katika taasisi zinazofuatilia kesi hizo.

Ofisa ufuatiliaji na tathmini kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Ofisi Zanzibar, Mohammed Khatib Mohammmed, alisema hayo wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari katika Ofisi za Tamwa, mjini hapa.

Alisema katika kufikia malengo ya kukomeshwa kwa vitendo hivyo ni lazima taasisi za habari kuwa na utaratibu wa kuandika takwimu sahihi za matukio ya udhalilishaji ili kuwa rahisi kuzifuatilia kesi zinazotokea na kujua mwendelezo wa kesi hizo.

Mohammed alisema waandishi wa habari wana kazi kubwa katika jamii ya kutoa elimu ya vitendo hivyo ambavyo vimekuwa sugu na kuliathiri taifa.

Alisema iwapo kila chombo cha habari kitakuwa na takwimu za matukio ya udhalilishaji, inawezekana ikawa njia imara ya ufuatiliaji wa kesi ambazo ziko mahakamani na mwendelezo wake.

Alisema hivi sasa waandishi wengi wanaripoti matukio ya udhalilishaji yanapotokea, lakini changamoto ipo katika kuzifuatilia kesi hizo zinapokuwa mahakamani.

Alisema wakati umefika kwa jamii kuachana na rushwa na usiri kwa wanaofanya vitendo hivyo na badala yake kuziripoti katika vyombo husika ili sheria ichukue mkondo wake.

Kwa upande wao wahariri wa vyombo vya habari walisema katika kufikia malengo ya kuwa na takwimu za matukio hayo ni lazima taasisi hizo zifanye kazi za ziada za ufuatiliaji wa matukio ya udhalilishaji.

# RC Tabora ataka orodha vigogo biashara haramu

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amemtaka Mrajisi Msaidizi wa Ushirika wa mkoa huo kupeleka ofisini kwake majina ya watumishi na viongozi wanajihusisha na biashara haramu ya mazao ya biashara, ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Alitoa agizo hilo wakati wa Kikao cha Ushauri cha Mkoa (RCC) cha kupitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Alisema vitendo hivyo ni tatizo kwa wakulima na vinawafanya waendelee kuwa maskini na halmashauri za wilaya kupata mapato kidogo ya ushuru wa mazao.

Mwanri alisema haiwezekani kila wakati Ofisi ya Mrajisi Msaidizi inatoa taarifa kuwa kuna baadhi ya viongozi wa serikali, wa kisiasa na vyama vya ushirika wamejiingiza kwenye biashara ya vishada na uuzaji wa pembejeo bila kuwataja majina.

Alisema serikali kupitia Waziri Mkuu ilishatoa maelekezo kuwa mtu akayeruhusiwa kuuza tumbaku ni yule ambaye ana shamba la tumbaku na zao hilo litauzwa kupitia ushirika.

Kamati hiyo iliviomba vyombo vya ulinzi na usalama, ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuchunguza na kuwafuatilia wanaojihusisha na vitendo hivyo ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Ilisema vitendo hivyo ni kosa kutokana na wahusika kutoa rushwa na udanganyifu kwa ajili ya kumnyonya mkulima na kuibia serikali mapato yake yanatokana na ushuru wa mazao.

Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, alisema kuna baadhi ya viongozi wanashiriki katika biashara chafu ya uuzaji ya ukopeshaji wa fedha kwa wakulima kwa riba kubwa na kuwafanya kuendelea kuwa maskini.

Alisema kuna baadhi ya wakulima wamekuwa wakikopeshwa pembejeo na fedha kwa mara mbili ya bei halali kwa madai kuwa pindi watakapovuna tumbaku, ni lazima wampe sehemu ya tumbaku kama malipo ya deni.

Makungu alisema vitendo hivyo vimefanya wakulima wengi wakati wa kuuza tumbaku yao kubaki na fedha kidogo na sehemu kubwa ya mauzo inaenda kwenye deni.




Mtaalamu wa Huduma za Kidijitali wa Tigo Tanzania, Ikunda Ngowi (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 13, kwa mkazi wa Mbagala, Miller Said Kungwi, baada ya kuibuka mshindi wa promosheni ya Tigo Chemsha Bongo 2020, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Karagwe waomba taasisi utatuzi wa migogoro

**Na Restuta Damian,** KARAGWE

WANANCHI wilayani Karagwe mkoani Kagera, wameziomba taasisi, mashirika na sekta za umma kufanikisha utatuzi wa changamoto za upatikanaji wa haki katika migogoro mbalimbali ya kijamii.

Hatua hiyo imetokana na uwapo wa uhitaji wa msaada na haki kutokana na jamii kuwa na migogoro inayopelekea kuondoa uvunjifu wa amani.

Wakizungumza na Nipashe katika Siku ya Msaada wa Kisheria inayofanyika viwanja vya Whangalawe Kata ya Kayanga wilayani hapa, Emmanuel Ilomba mkazi wa Kijiji Nyabugwegira, alisema kuna matukio mengi hasa mauaji na unyang'aji wa ardhi, ambayo wananchi wanaogopa kutoka taarifa kwa kuogopa vitisho.

Ilomba alisema matukio hayo yanakwama kufika katika mamlaka husika kutokana na gharama kwani kuna umbali mrefu licha ya kuhitaji msaada wa kujua sheria na haki.

Akwilina Kazuri, mkazi wa Kijiji cha Bugene Kata ya Bugene, alisema ujio wa ofisi hizo kwa ajili ya kusikiliza wananchi inayonyesha wazi kuwa dhuluma ya ardhi na mirathi itaondoka.

Alisema shida kubwa ni mashamba yanayoingiliwa na watu kwa njia ya kununua bila kujua ni mali za ukoo wa familia fulani au dhuluma ya nguvu.

"Kwa muda mrefu mtu anatumia muda kutembelea ofisi na kushinda huko bila kupata nafasi ya kusikilizwa wala kuona mhusika na kupata ufumbuzi ni mateso makubwa," alisema Kaziri. Mkuu wa Kitengo cha Shirika la linalotoa Huduma kwa wanawake MHOLA, Teresia Bujiku, alisema makundi ya wanawake ndio yenye changamoto zaidi kwa upande wa mirathi na ndoa.

Alisema kesi nyingi ambazo hufika kwenye shirika hilo zinahusu ardhi ambapo kwa mwaka 2019 waliweza kufikia wananchi 7,808 kati ya walengwa 14,200.

Aliongeza kuwa kesi 795 zilihusisha mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii na kupitia mikutano ya hadhara, iliweza kufika wananchi 2,000 kwa mwaka.

Mwanasheria wa wilayani Karagwe, Samara Matiko, alisema kama wananchi watajengewa uelewa kupitia siku ya msaada wa kisheria, kuna uwezekano wa kupunguza migogoro na msongamano maofisini.

Matiko alisema shughuli inayofanyika kwa wiki hiyo ni kuangalia jinsi ya kutafuta na kumpatia mwananchi msaada wa kisheria.

Naye Mkuu wa Mkoa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema mkoa kwa kushirikiana na mashirika ya TANRAP na MHOLA kwa yalifadhi siku hiyo, yamekuwa yakisaidiana na serikali kutatua changamoto hizo.

Gaguti alisema lengo ni kupunguza msongamano kwenye ofisi pamoja na kupunguza gharama kwa mwananchi kwa kuwa kuna zaidi ya taasisi 30 zitahudumia wananchi.

## Bakita, Bakiza zapewa tano kukuza Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimepongeza Baraza la Kiswahili Tanzania (Bakita) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (Bakiza) kwa kazi kubwa waliyofanya katika kuandaa waraka wa ushawishi wa kuingiza Kiswahili kama moja ya lugha rasmi ya mawasiliano katika nchi za SADC.

Pongezi hizo zimetolewa katika kikao cha ushirikiano baina ya Wizara zenye dhamana ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kati ya Serikali ya Jamahuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ngazi ya makatibu wakuu kilichofanyika Zanzibar Machi 03, 2020.

Akizungumza katika kikao hicho ngazi ya Makatibu Wakuu Mwenyekiti ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Saleh Yusuf Mnemo, amesema kuwa BAKITA na BAKIZA zimefanya juhudi kubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili ambayo ni nguzo muhimu katika kudumisha muungano wetu.

"Mabaraza haya mawili yanafanya kazi kubwa sana katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili ni lazima tuyapongeze lakini ni vizuri yakaendelea kushirikiana katika kuelimisha Watanzania matumizi mazuri na sahihi ya lugha hiyo ili iendelee kuwa miongoni mwa lugha bora duniani," alisema Saleh Yusuf.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Ally Possi ameyataka mabaraza hayo kuendelea kutafuta namna bora zaidi ya kukuza lugha hiyo nje ya nchi kwa kutumia fursa za uhitaji wa watalaam wa lugha hiyo zinazojitokeza kwa kuwa tayari ina kanzidata ya wataalamu hao.

"Sekta hizi zina umuhimu mkubwa katika Muungano wetu ni vizuri wakuu wa idara na taasisi kuwa na utaratibu wa kukutana angalau mara moja kwa mwaka ili kujadili utekelezaji wa maazimio ya maeneo ya ushirikiano pamoja na kutatua changamoto ambazo zinajitokeza kabla mamlaka za juu hazijafanya hivyo," alisema Dk. Possi.

# HABARI KIMATAIFA

## Mgonjwa wa mwisho wa ebola atoka hospitali

**KINSHASA,** Congo

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hakuna mgonjwa yoyote anayeugua ugonjwa wa ebola.

Hatua hiyo imekuja baada ya kupona kwa mgonjwa wa mwisho aliyelazwa hospitalini mji wa Beni ulio kaskazini-mashariki mwa nchi hiyo.

Kiongozi wa kikanda wa WHO, Dk. Mathsidiso Moeti alielezea kwenye akaunti yake ya mtandao wa kijamii wa Twitter kuwa wamepokea kwa tahadhari matarajio ya matokeo mazuri hayo kuhusu ugonjwa huo uliotangazwa rasmi Agosti mosi, 2018.

Ugonjwa wa ebola nchini Congo utatangazwa kuwa umemalizika endapo hakutokuwapo na kisa kipya kwa muda wa siku 42.

Hadi kufikia jana ni siku 15 imetimia ambayo hakujaorodheshwa kisa kipya cha ugonjwa huo wa ebola kwenye majimbo ya Kivu ya Kaskazini na Ituri, ilielezea taarifa ya Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Mgonjwa wa mwisho aliyepona aliondoka jana kwenye kituo cha matibabu ya ebola cha Beni, eneo la mwisho lililokumbwa na ugonjwa huo mashariki mwa Congo.

Mwanamama huyo, Masika Mawasu Semida, alipongeza wauguzi kwa huduma aliyopewa.

Watu 2,264 walikufa kutokana na ugonjwa wa ebola huko Beni na Ituri, ambao ni kwa mara ya 10 Congo kukumbwa na ugonjwa huo hatari toka mwaka 1976. **DW**

## Waziri Mkuu ajiuzulu baada ya miezi sita

**KYIV,** Ukraine

WAZIRI Mkuu wa Ukraine, Oleksiy Honcharuk, amewasilisha barua ya kujiuzulu kwa mara ya pili katika kipindi cha miezi miwili.

Wabunge kutoka chama tawala ndiyo watakaoamua kama watakubali kujiuzulu kwake au la wakati wa kikao maalumu.

Waziri wa Fedha na Mambo ya Nje huenda pia wakaondolewa katika nyadhifa zao kama sehemu ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri.

Naibu Waziri Mkuu, Denys Shmygal, anapigiwa upatu kuchukua nafasi ya Honcharuk. Shmygal awali alihudumu kama mkuu wa utawala wa kikanda katika Jimbo la Magharibi la Ivano-Frankvisk kabla ya kuchukua wadhifa wa naibu waziri mkuu mwezi uliopita. **DW**

# Wafungwa 54,000 waachiwa kuepuka maambukizi corona

**TEHRAN,** Iran

IRAN imewaachia huru kwa muda wafungwa zaidi ya 54,000 ikiwa ni miongoni ma jitihada za kukabiliana na maambulizi ya virusi vya ugonjwa wa corona katika magereza yaliyo na msonganamo wa watu.

Msemaji wa mahakama, Gholamhossein Esmaili, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wafungwa waliruhusiwa kutoka gerezani baada ya kupimwa na kukutwa hawana ugonjwa wa Covid-19.

Hata hivyo, wafungwa wa usalama waliofungwa kwa muda wa zaidi ya miaka mitano hawataachiwa.

Mfanyakazi wa wahitaji nchini Iran ambaye ni raia wa Uingereza, Nazanin Zaghari-Ratcliffe anaweza kutolewa hivi karibuni kwa mujibu wa mbunge wa Uingereza.

Balozi wa Uingereza nchini Iran, Tulip Siddiq, alisema kuwa Zaghari-Ratcliffe ataachiwa huru muda wowote. Mume wake alisema Jumamosi kuwa aliamini mke wake alipata maambukizi ya Covid-19 akiwa Gereza la Evin laTehran na mamlaka iliyokuwa inakataa kumpima.

**Zaghari-Ratcliffe alifungwa kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2016 baada ya kukamatwa alikanusha kuhusika na madai yanayomkabili.**



Esmaili alisisitiza Jumatatu kuwa Zaghari-Ratcliffe alikuwa akiwasiliana na familia yake na kuwaambia kuwa afya yake iko salama.

Zaghari-Ratcliffe alifungwa kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2016 baada ya kukamatwa alikanusha kuhusika na madai yanayomkabili.

Msemaji wa Ofisi ya Mambo ya Nje alisema kuwa serikali ya Iran itawaruhusu haraka wataalamu wa afya kuingia katika Gereza la Evin kuangalia hali za raia wenye uraia wa Uingereza na Iran zikoje.

Mpaka sasa zaidi ya matukio 90,000 ya ugonjwa wa Covid-19 duniani kote yameripotiwa na vifo 3,110 vimetokea tangu ugonjwa huu uanze mwishoni mwa mwaka jana, huku wengi waliokufa ni Wachina.

Mlipuko wa virusi vya corona umeua watu wapatao 77 nchini Iran katika kipindi cha wiki mbili. **BBC**




Bernie Sanders (kushoto) na Joe Bien wakati wa mjadala kati ya wagombea wa urais katika kura za mchujo katika chama cha Democratic huko Charleston, South Carolina. **PICHA: AFP**

# Biden, Sanders 'wakabana koo' uchaguzi

**WASHINGTON,** Marekani

MATOKEO ya kwanza ya kuhusu kura za mchujo kwa wagombea urais katika chama cha Democratic yanaendelea kutolewa kwa upande mmoja baada ya mwingine.

Kura zimepigwa katika majimbo 14 ili kumchagua mgombea atakayepambana na Rais Donald Trump katika uchaguzi wa urais uliopangwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Wagombea katika uchaguzi huo ni kati ya Seneta kutoka Vermont, Bernie Sanders, Makamu wa Rais wa zamani na Joe Biden. Biden amenyakua ushindi katika majimbo ya Alabama, Arkansas, North Caroline, Massachusetts, Minnesota, Oklahoma, Tennessee na Virginia.

Naye Sanders anaongoza katika majimbo ya Colorado, Utah na Vermont. Hivi sasa ndiye anaongoza katika majimbo ya California na Texas.

Kwa upande mwingine Elizabeth Warren ameanguka katika ngome yake ya Massachussets, huku Joe Biden akiibuka mshindi katika jimbo hilo, kulingana na taarifa za vyombo vya habari vya Marekani.

Makamu wa rais wa zamani, ambaye hadi hivi sasa anakabiliwa na upinzani mkubwa tangu kuanza kwa kura hizi za mchujo, amefanya vizuri katika majimbo nane wakati wa zoezi hilo la "Jumanne maalum", ambapo kwa jumla majimbo 14 yamepiga kura.

Jumla ya wajumbe 1,357 wanashindaniwa katika uchaguzi huu wa Jumanne Maalum na Biden anahitaji matokeo mazuri ili kumzuia Sanders kuchukua uongozi mkubwa kabla ya mkutano mkuu wa chama utakaomteua mgombea wa chama Julai.

Wengi katika chama cha Democratic wana hamu ya kuizuia kasi ya Sanders katika kura hizo za wajumbe, wakisema seneta huyo atashindwa vibaya kabisa katika uchaguzi mkuu ambao Rais Trump amedokeza kuwa atamuita kuwa msoshalisti anayetaka kuuwekea kikomo mtindo wa maisha ya Wamarekani.

Meya wa zamani wa New York, Michael Bloomberg na Seneta wa Massachusetts Elizabeth Warren pia wanashiriki katika kinyang'anyiro hiki. **RFI**

# NMB yapiga jeki vifaa elimu, afya Dar, K'jaro

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekabidhi misaada mbalimbali ya vifaa tiba na vifaa vya elimu katika mikoa ya Dar es Salaam na Kilimanjaro, ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa kurejesha kwa jamii asilimia moja ya faida yao kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR).

Jijini Dar es Salaam, NMB imetoa misaada yenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa Shule ya Sekondari Tambaza, iliyopo Upanga na Kituo cha Afya Pugu Kajiungeni wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, wakati mkoani Kilimanjaro imekabidhi vifaa tiba kwa Hospitali ya Wilaya ya Hai.

Tambaza Sekondari, imepokea msaada wa vitanda 80 vya kulalia wasichana wa shule hiyo vyenye thamani ya Sh. milioni 10, vilivyokabidhiwa na Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd na kupokelewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu.

Katika hafla ya kukabidhi vifaa tiba katika Kituo cha Afya Pugu Kajiungeni, NMB ilikabidhi msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 5 kupitia kwa Meneja Mwandamizi wa NMB Kitengo cha Biashara za Serikali, Adelard Mang'ombo na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sofia Mjema.

Mkoani Kilimanjaro, NMB kupitia Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, alikabidhi msaada wa vitanda vitano vya kulalia, viwili vya kujifungulia kinamama, mashuka 25, magodoro 5, pamoja na hundi ya Sh. 16 za wakulima wa zao la vanilla mkoani humo.

Muro akiwa ameambatana na Meneja wa NMB Tawi la Hai, Medard Malisa, alikabidhi vifaa tiba hivyo kwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Hai, Agnes Hokororo, tukio lililoshuhudiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai, Yohana Sintoo.

Akizungumza wakati akipokea vitanda kwa ajili ya bweni la wasichana Tambaza Sekondari, Zungu, ambaye ni Mbunge wa Ilala, alikiri kuwa mabadiliko chanya katika Sekta ya Elimu na Afya, yanahitaji nguvu za pamoja baina ya serikali na wadau muhimu kama Benki ya NMB.

Zungu aliipongeza NMB kwa namna inavyojitoa kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha sekta za elimu na afya, kwa aina ya misaada inayotoa kila wakati kupitia kitengo chake cha CSR.

Kwa upande wake, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Idd, aliushukuru uongozi wa Tambaza Sekondari kwa kuwafikiria wao walipohitaji msaada wa vitanda na kwamba wanajisikia faraja kuendelea kuwa sehemu ya utatuzi wa changamoto za shule hiyo kongwe.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Tambaza Sekondari, Dk. Amos Mwakilasa, aliishukuru NMB kwa msaada huo, unaoenda kumaliza changamoto ya malazi miongoni mwa wasichana wa shule hiyo, yenye jumla ya wanafunzi wa kike na kiume wapatao 760.

Katika hafla ya kukabidhi vifaa tiba kwa Kituo cha Afya Pugu, Meneja Mwandamizi wa NMB Kitengo cha Biashara za Serikali, Adelard, alisema afya kwa jamii ni nguzo kuu ya maendeleo kwa taifa lolote, ndio maana NMB imekuwa ikitoa kipaumbele kukabiliana na changamoto hizo pale inaposhirikishwa.



Magari yakipita kwa tabu kwenye maji yaliyotuama katika eneo la Akiba, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ruvuma yajipanga kukabiliana corona

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amewaomba viongozi mbalimbali wa dini mkoani humo kutumia nyumba za ibada kuliombea taifa ili Mwenyezi Mungu aliepusha na ugonjwa wa corona.

Mndeme ametoa rai hiyo hivi karibuni wakati alipokuwa akizungumza katika warsha ya viongozi wa mkoa na wilaya kuhusu mpango wa usajili watoto walio na umri chini ya miaka mitano, iliyofanyika mjini hapa.

Alisema viongozi wa dini wanapaswa kutumia nyumba za ibada kwa ajili ya kuliombea taifa ili Mwenyezi Mungu alinusuru na ugonjwa huo.

Alisema kuwa katika kukabiliana na changamoto ya ugonjwa huo, ameziagiza halmashauri zote mkoani humo kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wananchi watakaogundulika kuwa na ugonjwa huo.

Alisema Mkoa wa Ruvuma upo salama kwa kuwa mpaka sasa hakuna mwananchi yeyote aliyegundulika kuwa na ugonjwa huo.

Mndeme aliwataka wananchi kunawa mikono kwa maji yanayotembea na yaliyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

Aliwatahadharisha wananchi wa mkoa huo kuachana na utamaduni wa kusalimiana kwa kupeana mikono na kukumbatiana.

**Viongozi wa dini wanapaswa kutumia nyumba za ibada kwa ajili ya kuliombea taifa ili Mwenyezi Mungu alinusuru na ugonjwa huo.**

# Mvutano wa kujenga makao makuu Bunda wamalizwa

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MVUTANO kati ya madiwani wa Jimbo la Bunda na Jimbo la Mwibara, mkoani Mara umefikia mwafaka baada ya Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Bunda kupitisha azimio la kujengwa makao makuu ya halmashauri hiyo eneo la Mwibara.

Kabla ya kupitishwa kwa azimio hilo, kila upande ulitaka ofisi za makao makuu ya halmashauri hiyo zijengwe katika jimbo lao.

Hatua hiyo iliwahusisha watendaji wa halmashauri kujiingiza katika masuala ya kisiasa na kupendelea upande fulani.

Katika kikao hicho, madiwani wa pande zote mbili walipambana kwa hoja kutetea maslahi ya wananchi wao.

Madiwani wa kutoka Jimbo la Bunda, ambalo mbunge wake ni Boniphace Getere, walisema kuwa makao makuu yanapaswa kujengwa katika jimbo hilo kwa sababu kuna vigezo vya msingi vikiwamo vyanzo vingi vya mapato na kuwapo kwa hospitali ya halmashauri hiyo.

"Mwenyekiti tunaomba makao makuu ya halmashauri ya wilaya yetu ya Bunda yajengwe katika Jimbo la Bunda, kwa sababu kuna hoja nyingi za msingi ikiwamo ya vyanzo vingi vya mapato kuwa vipo katika jimbo hilo na pia kuna Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda," alisema Diwani Fyeka Sumera wa Nyamuswa.

Diwani wa Namhura Jogoro Amoni, kutoka katika Jimbo la Mwibara, alisema makao makuu ya halmashauri yanapaswa kujengwa katika mji wa Kibara katika Jimbo la Mwibara ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Jogoro alisema kwa sasa ofisi za makao makuu ya halmashauri hiyo ziko katika eneo la mji wa Kibara, tangu Rais Dk. John Magufuli, alipotoa tamko kwamba halmashauri zote nchini zisogeze huduma kwa wananchi," alisema Jogoro akiungwa mkono na madiwani wote wa jimbo hilo.

Wabunge wa majimbo hayo, Getere wa Jimbo la Bunda na Kangi Lugola wa Mwibara, kila mmoja alitaka kusogeza huduma za serikali karibu na wananchi, hali iliyofanya kuwapo mvutano kikao hicho.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri, Amos Kusaja, akitoa ufafanuzi wa jambo hilo alisema, mapendekezo ya kwanza yalizingatia ushauri wa watendaji na wataalamu wa halmashauri hiyo.

Kufuatia malumbano hao, mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Isack Maela, aliamuru zipigwe kura na ndipo ikaamuriwa kuwa makao makuu yajengwe katika Jimbo la Mwibara.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alisema, serikali inawapenda watumishi wake na wakatekeleza majukumu yao ipasavyo bila kuingiza mambo ya siasa.

# KLOPP: SIJAUMIZWA NA KICHAPO CHELSEA



**LONDON,** England

KOCHA Jurgen Klopp amesema matokeo ya juzi usiku iliyopata Liverpool kwa kufungwa na Chelsea hayajamuumiza.

Kocha huyo alisema alipata maumivu baada ya kupoteza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Watford.

Kauli ya Klopp imekuja baada ya Liverpool kufungwa mabao 2-0 na Chelsea katika mchezo wa Kombe la FA raundi ya tano na hivyo kutupwa nje kwenye mashindano hayo na kufuta ndoto zake za kubeba mataji matatu msimu huu.

Mabao ya Ross Barkley na Willian yalitosha kuendeleza kipigo kwa timu hiyo katika mechi tatu kati ya nne za mwisho ilizocheza hivi karibuni.

Awali, Liverpool ilipoteza kwa kufungwa na Atletico Madrid katika mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, halafu ikafungwa na Watford kabla ya juzi usiku kukubali kipigo kingine kutoka kwa Chelsea.

Liverpool ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Metropolitano ilifungwa bao 1-0 kabla ya kuchapwa 2-0 dhidi ya Watford. Klopp alisema kati ya mechi hizo tatu, aliumizwa zaidi na kipigo cha Watford.

# Wanyama amfuata Henry Marekani

**LONDON,** England

KIUNGO wa Tottenham, Victor Wanyama amesaini mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Montreal Impact, imethibitishwa jana.

Wanyama mwenye umri wa miaka 28, alicheza mechi nne kweye mashindano yote kwa Spurs msimu huu wa 2019-20 na sasa atajiunga na Thierry Henry pale Montreal kwa uhamisho huru.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Kenya, alitua Tottenham akitokea Southampton mwaka 2016 na atacheza nje ya Ulaya kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka.

"Kwa uhakika nina furaha kujiunga na klabu kama Montreal Impact," alisema Wanyama katika taarifa yake.

"MLS inaendelea kukua kila msimu na naangalia uwezekano wa kuitangaza zaidi barani Afrika.

"Nilipozungumza na Thierry aliniambia alinitaka niungane naye pale Montreal, na sikufikiria mara mbili.

"Mara zote amekuwa mchezaji ambaye navutiwa naye, na kwa uhakika nina furaha kupata nafasi ya kucheza Montreal Impact."

Montreal ilishinda mchezo wake wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya Marekani msimu huu dhidi ya Dallas, Jumamosi.







# Sancho sasa kujazwa noti abaki Dortmund

**DORTMUND,** Ujerumani

OFISA Mtendaji wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke haamini kama Jadon Sancho anataka kuondoka kwa miamba hao wa Bundesliga baada ya kuhusishwa na mpango wa kwenda Manchester United.

United imeripotiwa kwamba inawania kumsajili nyota huyo wa Dortmund na timu ya Taifa ya England, Sancho mwishoni mwa msimu huku, huku pia vinara wa Ligi Kuu ya England, Liverpool na Chelsea zote zikimuwania.

Wakati uvumi huo kuhusu majaliwa ya Sancho ukipamba moto, Watzke - ambaye amebainisha "hana uhakika na kitakachotokea," amesisitiza Dortmund ina fedha za kutosha kuweza kumpa ofa nene mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19.

"Nafikiri anahisi kwamba klabu haina majaliwa mazuri ya baadaye," amesema Watzke akinukuliwa na BBC Sport. "Kwa maoni yangu, sidhani kama anataka kuondoka."

"Si swali kuhusu fedha," amesema Watzke. "Kwa upande wetu, litakuwa jambo bora kama atabakia Borussia Dortmund.

"Tuna fedha za kutosha. Tunataka kupata mataji. Nafikiri timu hii ina nafasi nzuri zaidi kuwa na Jadon kuliko kumkosa."

Watzke aliongeza: "Tuna siri kubwa ya mahusiano kati yake na sisi pamoja na wakala wake. Tutalijadili hilo."

HABARI MICHEZO

# Flick akunwa Bayern nusu fainali DFB-Pokal

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick ameridhishwa na kiwango cha timu yake baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Schalke 1-0 kwenye robo fainali ya Kombe la Ujerumani (DFB-Pokal).

Bao la Joshua Kimmich la dakika ya 40, lilitosha kwa Bayern kutawala mchezo huo kwenye Uwanja wa Veltins Arena, Jumanne.

Licha ya ushindi huo mwembamba, Flick alikuwa na furaha kwa Bayern kutinga robo fainali kwenye michuano hiyo ya DFB-Pokal.

"Timu yangu ilicheza vizuri sana. Nimeridhishwa na namna tulivyoshinda mchezo," alisema baada ya mchezo huo.

"Tulicheza dhidi ya Schalke timu ambayo inacheza vizuri zaidi kwenye safu yake ya ulinzi. Tulitengeneza nafasi na kwa ujumla tulicheza vizuri kwa asilimia 80.

"Mwisho wa siku, mara zote ni muhimu kuona kwamba tunasonga mbele kwenye mashindano haya. Tupo kwenye nusu fainali, najivunia timu yangu. Wachezaji wameonyesha morali ya hali ya juu na wapo kwenye kiwango kizuri."

Vinara hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern wanaongoza msimamo wa ligi hiyo na Jumapili watacheza na Augsburg.





# ARTETA KURUDI KWA GUARDIOLA MACHI 11

**LONDON,** England

MCHEZO wa Ligi Kuu ya England kati ya Manchester City dhidi ya Arsenal umepangwa kupigwa Jumatano ijayo Machi 11, mwaka huu.

Arsenal awali walikuwa wamepangwa kwenda pale Uwanja wa Etihad wikendi iliyopita, lakini Man City walikuwa wanacheza fainali ya Kombe la EFL na hivyo kulazimika kuahirishwa.

Mikel Arteta timu yake itacheza dhidi ya City kwa mara ya kwanza tangu alipoondoka kama msaidizi wa Pep Guardiola kuchukua mikoba hiyo ya kuwanoa 'Washikabunduki' hao.

City, ambao wametwaa taji la EFL kwa msimu wa tatu mfululizo baada ya kuifunga Aston Villa 2-1 pale kwenye dimba la Wembley, ilishinda 3-0 kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Arsenal uliopigwa pale Uwanja wa Emirates, Desemba mwaka jana.

Arsenal wapo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu na wamepitwa pointi nane na Chelsea waliopo nafasi ya nne na mchezo mmoja mkononi, huku City wapo nafasi ya pili wakipitwa pointi 22 na vinara Liverpool.

Kikosi hicho cha Guardiola jana Jumatano kilishuka dimbani kucheza na Sheffield Wednesday kwenye mchezo wa raundi ya tano wa Kombe la FA, kabla ya kwenda kucheza na Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford Jumapili.

# *Corona yaahirisha mechi ya Juve*

**TURIN,** Italia

MCHEZO wa pili wa nusu fainali ya Kombe la Italia kati ya Juventus na AC Milan uliotakiwa kupigwa jana Jumatano hapa Turin, umeahirishwa kwa sababu ya hofu ya ugonjwa wa corona.

Hiyo ni baada ya kuripotiwa kwamba watu 27 wamefariki duniani kutokana na ugonjwa huo nchini Italia ndani ya saa 24, na kufanya idadi yake kufikia watu 79.

Matukio ya michezo yalizuiwa katika mikoa mitatu, Lombardy, Veneto na Emilia Romagna pamoja na miji mingine miwili.

"Mchezo umeahirishwa na tarehe mpya itatangazwa baadaye," ilisema taarifa ya Juve.

Timu hizo mbili zilitakiwa kukutana kwenye Uwanja wa Allianz Arena baada ya mchezo wa kwanza kumalizika kwa matokeo ya 1-1 baada ya Cristiano Ronaldo kufunga penalti ya dakika za majeruhi kuipa sare hiyo Juve.

Napoli nao watacheza na Inter Milan kwenye mchezo wa Coppa Italia leo Alhamisi.

Mechi nne tu za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, zilipigwa wikendi iliyopita, huku ligi yote ya nchini Uswisi ikiahirishwa hadi Machi 23.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE AMTAJA KANE NA RASHFORD EURO 2020

### ●●● Pia amtaka Vardy kufungua milango ya kurejeshwa kuitumikia England huku akieleza...

**LONDON,** England

KOCHA wa England, Gareth Southgate amewataja washambuliaji wake wawili Harry Kane na Marcus Rashford kuwa ana matumaini makubwa watakuwa fiti kwa ajili ya michuano ya Euro 2020.

**Straika huyo wa Tottenham, Kane amekuwa nje ya uwanja tangu Januari Mosi akiuguza majeraha ya misuli, wakati mshambuliaji wa Manchester United, Rashford amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mgongo.**

"Wote wakiwa vizuri watakuwamo kwa ajili yetu majira ya joto," alisema Southgate.

Kocha huyo wa England pia hajaweka kando suala la kumtaka mshambuliaji wa Leicester, Jamie Vardy kuruhusu yeye mwenyewe kuitwa katika kikosi hicho.

Vardy alijiweka kando kutoka katika soka la kimataifa mwaka 2018, wakati huo akisema "ikiwa mbaya zaidi ilitokea na kila mtu alijeruhiwa, basi ni wazi nisingesema hapana".

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ni miongoni mwa wachezaji wanaoongoza kwa ufungaji wa mabao Ligi Kuu England msimu huu wakiwa na mabao 17.

"Kwa nini nimweke mtu yeyote nje?" Alisema Southgate." Mara zote nimesema kuwa mlango kamwe haujafungwa."

Rashford, ambaye hajacheza tangu Januari 15, amefunga mabao 14 kwenye ligi msimu huu, wakati Kane akiwa akicheka na nyavu mara 11.

"Mimi ni mkweli," aliongeza Southgate. "Ninawaza kuhusu Harry Kane na Marcus Rashford, wote walikuwa na majeraha makubwa, lakini wote kati yao watafanya kila kitu ndani ya nguvu zao kujiwezesha wenyewe kuwa fiti na tayari kwetu majira ya joto.

"Kipaumbele cha kwanza kwao wote ni kurejea kuzichezea klabu zao."

England itaanza kutupa karata yao ya kwanza kwenye michuano ya Euro 2020 dhidi ya Croatia katika Uwanja wa Wembley Juni 14, mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### BARCA, LIVER KWA TORRES

BARCELONA imejiunga na Liverpool na Real Madrid katika mbio za kumsajili winga wa Valencia, Ferran Torres, 20. ***(El Mundo Deportivo via Daily Mail)***

### POCHETTINO KUMRITHI ZIDANE

REAL Madrid imemtaka kocha wa zamani wa Spurs, Mauricio Pochettino kuendelea kuijulisha mipango yake wakati huu ikizingatia kumnasa kwa ajili ya kurithi mikopa Zinedine Zidane. ***(Independent)***

### INTER YAMFUNGUKIA SANCHEZ

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez, 31, atahitajika kushusha mshahara wake kama atataka kukamilisha mchakato wa kuhamia jumla Inter Milan majira ya joto. ***(Tuttosport via Daily Mail)***

### JUDE KUIGHARIMU DORTMUND

KIUNGO wa Birmingham City na England U-17, Jude Bellingham, 16, anajiandaa kuweka rekodi ya usajili Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 30.4. ***(Bild - in German)***

### KANE KUITOA JASHO SPURS

TOTTENHAM itakabiliwa na vita kali ya kumbakisha straika wake kinara, Harry Kane, 26, katika majira ya joto kama itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Telegraph)***

### VILLA MGUU SAWA KWA SANSON

ASTON Villa inavutiwa na kiungo wa Marseille, Morgan Sanson, 25, lakini inajua nafasi yao ya kumsajili nyota huyo wa zamani wa Ufaransa U-21 kunategemea endapo itabaki Ligi Kuu England msimu ujao. ***(Birmingham Mail)***

### BRUCE AKANA BIFU NA ALLAN

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce amesema taarifa ya kuwapo kwa mpasuko kati yake na mshambuliaji Mfaransa, Allan Saint-Maximin, 22, ambaye anahusishwa na kujiunga na Wolves, "kwa ujumla ni upuuzi". ***(Newcastle Chronicle)***

### ATLETICO MBIO KWA RAKITIC

ATLETICO Madrid ipo mstari wa mbele katika mchakato wa kumsajili kiungo wa Barcelona, Ivan Rakitic, 31, na wakati nyota huyo wa kimataifa wa Croatia akiwa tayari kubaki Hispania. ***(Marca)***

### FOSTER AIKANA TOTTENHAM

KIPA wa Watford, Ben Foster amesema uhamisho wa kwenda Tottenham majira ya joto ni "habari za magazeti". Nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa England, 36, yupo atamaliza mkataba wake majira ya joto. ***(Watford Observer)***

### MOURINHO HATAIBOMOA SPURS

KOCHA Spurs, Jose Mourinho amesema hajapanga kukifanyia mabadiliko kikosi chake majira ya joto. ***(Evening Standard)***

### GERRARD ATOA MSIMAMO

KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard amesema ataondoka katika klabu hiyo endapo tu atatimuliwa. ***(The Scotsman)***

HABARI MICHEZO

## Kungwi ashinda Tigo Chemsha

**Na Mary Geofrey**

MKAZI wa Mbagala jijini Dar es Salaam, Miller Kungwi amejinyakulia zawadi ya Sh. milioni 13 baada ya kuibuka mshindi wa Promosheni ya Tigo Chemsha Bongo 2020.

Promosheni hiyo ilidumu kwa miezi mitatu na wateja wa Tigo walipata nafasi ya kujishindia zawadi za pesa taslim kila siku na droo ya mwisho mshindi alikuwa anajinyakulia zawadi ya Sh. milioni 13.

Washindi 90 kila siku walijishindia Sh. 100,000 na walipatikana washindi 12 kili wiki kwa muda wa wiki 12.

Akizungumza wakati akikabidhiwa hundi ya fedha hizo, Kungwi alisema alishuhudia kuona washindi mbalimbali, lakini hakuwahi kudhani angekuja kubahatika kama ilivyotokea.

"Wakati napigiwa simu,nilikuwa nyumbani najipanga kutoka kwenda katika mihangaiko yangu ya kibiashara, basi nilipopata ile taarifa kwamba nimeibuka mshindi nilifurahi sana kwani sikutegemea kabisa kuwa ningeibuka mshindi katika promosheni hii," alisema Kungwi.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Huduma za Kidijitali kutoka Tigo, Ikunda Ngowi, alimpongeza mshindi huyo na kutumia fursa hiyo kuwashukuru wateja wote wa kampuni ambao walishiriki na baadhi yao kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo zawadi za fedha taslimu.

## Mbao yasisitiza haishuki daraja

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Yanga, Kocha Msaidizi wa Mbao FC, Agustino Malindi, amesema bado hawajakata tamaa na badala yake wataendelea kupambana ili wasishuke daraja.

Akizungumza na gazeti hili, Malindi alisema kikosi chake kilipoteza mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na wachezaji wa Yanga kucheza katika kiwango kizuri.

Malindi alisema walizidiwa uwezo katika mchezo huo, lakini makosa aliyoyaona atayafanyia kazi na kuahidi wataingia tofauti katika mechi yao dhidi ya KMC itakayochezwa keshokutwa, Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

"Ingawa tumefungwa na Yanga lakini hatukati tamaa, makosa tumeyaona na tutayarekebisha ili yasijitokeze tutakapokutana na KMC Jumamosi," alisema Malindi.

Aliongeza kuwa mchezo wao wa kesho ni muhimu kwa sababu anaamini wakipata ushindi, wachezaji wake wataimarika na kuanza kujiamini ili kupambana na hatimaye kubakia kwenye ligi hiyo.

# MASTRAIKA SIMBA WAMPASUA KICHWA EYMAEL AKIJIGAMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael amesema kikosi chake kimeimarika na hali hiyo inampa ujasiri wa kutarajia matokeo vizuri kuelekea mechi zinazofuata ukiwamo mchezo dhidi ya watani zao, Simba utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Juzi Yanga ilishinda mechi yake dhidi ya Mbao FC na huo ni ushindi wa pili mfululizo baada ya wiki iliyopita kuwafunga Alliance FC na kumaliza 'gundu' la sare lililokuwa limewang'ang'ania.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Eymael alisema anaamini uwezo wa wachezaji wake unazidi kukua kila siku jambo linalomfanya aondoe hofu na kuamini watafanya vizuri kwenye mechi zao zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Eymael alisema ana uzoefu mkubwa wa mechi za 'dabi' kwa mataifa ambayo aliyowahi kufundisha na mipango yake ni kuona wanashinda mechi hiyo.

"Hatuidharau Simba hasa katika safu yake ya ushambuliaji iko vizuri, kazi kubwa niliyokuwa nayo kwa sasa ni kuzuia balaa la washambuliaji wa Simba," alisema Eymael.

Kocha huyo alisema ana imani hilo litawezekana kutokana na kila siku wachezaji wake wanazidi kuimarika na kufanya kile ambacho anahitaji huku wakiwafurahisha pia mashabiki wa klabu hiyo.

"Sasa ninaona matokeo mazuri kwa vijana wangu, na hili linaleta mwanga wa kujua wapi tunakokwenda, hata kwenye mchezo wetu dhidi ya Simba tutafanya vizuri," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Alitaja tatizo alilolibaini kwa upande wa kikosi chake ni idadi ya mabao waliyonayo ni ndogo tofauti na Simba, kiasi ambacho kinamletea ugumu na kulazimika kufanyia kazi ili kuzuia balaa la wapinzani wao.

"Washambuliaji wangu wengi bado hawana umakini, wanapokuwa kwenye lango wanapoteza hali ya kujua nini wanatakiwa wafanye tofauti na wenzetu ambao wana washambuliaji wenye mabao mengi kuliko sisi," alisema Eymael.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga inaongozwa na Mkongomani David Molinga ambaye ana mabao saba wakati kwa upande wa Simba Mnyarwanda Meddie Kagere mwenye mabao 14 ndiye kinara wa ufungaji katika ligi hiyo.

POZA KOO...




Mkurugenzi Mkuu wa Tanga Cement, Reinhardt Swart (kulia), akiwapa maji baadhi ya wakimbiaji wa mbio za Kili Marathon 2020 kwenye kituo cha maji kilichoandaliwa na Kampuni ya Tanga Cement wakati wa mbio hizo zilizofanyika mwishoni mwa wiki mjini Moshi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tanapa yaendelea kuipiga 'tafu' Gofu*

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA la Hifadhi ya Taifa (Tanapa), limetangaza kudhamini mashindano ya gofu ya Klabu ya Lugalo ambayo yamepangwa kufanyika Machi 14 na 15, mwaka huu kwenye viwanja vya klabu hiyo jijini Dar es Salaam.

Mashindano hayo kwa mwaka huu yaliyopewa jina la 'Tanapa Lugalo Gofu' yanatarajiwa kushirikisha zaidi ya washiriki 100 ambao watakuwa katika madaraja mbalimbali.

Akizungumza jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu Lugalo, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luongo, alisema mashindano haya yataenda sambamba na ufunguzi wa ofisi za chama cha mchezo huo Tanzania (TGU) pamoja na Chama cha Gofu cha Wanawake nchini.

"Tunatarajia Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mwakyembe (Harrison) au mwakilishi wake atatufungia mashindano haya pamoja na kuzindua ofisi hizo ambazo zimejengwa na klabu ya Lugalo kwa kutambua umuhimu wa maendeleo ya mchezo huu," alisema Luongo.

Naye nahodha wa mchezo huo wa klabu ya Lugalo, Brown Masai, alisema mashindano hayo yatachezwa kwa mtindo wa 'Gross' ambapo mshindi wa jumla atatangazwa kuwa bingwa.

"Lakini tumegawa wachezaji kwenye makundi manne, kundi la wachezaji wa kulipwa, wachezaji wa ridhaa, wachezaji vijana na watoto ambapo kilele chake kitakuwa Machi 14," alisema Masai.

Alisema mashindano haya yatashirikisha wachezaji kutoka klabu mbalimbali zilizoko Tanzania Bara na Zanzibar.

Mwakilishi wa Tanapa, Hassan Mbaga, aliyemwakilisha Kamishna Mkuu alisema taasisi hiyo inaona fahari kutangaza hifadhi za Taifa kupitia michezo na wanaamini wataendelea kutumia fursa hiyo huku wakiwakutanisha wachezaji mbalimbali pamoja.

# Michezo

Alhamisi Machi 5, 2020

Nipashe




Southgate amtaja Kane, Rashford Euro UKURASA 30

MKOKO UMEWAKA...




Wachezaji wa Yanga, kutoka kushoto; David Molinga na Patrick Sibomana wakishangilia baada ya kupata bao dhidi ya Mbao FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi na timu yao kushinda 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Talib achambua dabi, Miquissone, Morrison

**Na Saada Salim**

ALIYEKUWA Kocha wa Simba, Talib Hilal amekichambua kikosi hicho na cha watani zao, Yanga kuelekea mechi ya dabi huku akiwagusa nyota wanaoongoza kwa mvuto katika klabu hizo, Luis Miquissone na Bernard Morrison.

Talib ambaye ni kocha wa timu ya Taifa ya soka la ufukweni nchini Oman aliwahi kuifundisha Simba kwa mafanikio na sasa ametoa tathmini yake juu ya mechi hiyo ya watani, Yanga dhidi ya Simba itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa akieleza timu yake hiyo ya zamani kiufundi ipo vizuri zaidi ya watani zao.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Hilal alisema kwa uzoefu wa michezo hiyo ana imani ufundi unakuwa mdogo huku wachezaji wakicheza kwa kukamiana na kuumizana.

Alisema kiufundi Simba iko vizuri kutokana na kwamba haitegemei mchezaji mmoja mmoja kama ilivyo kwa wapinzani wao, lakini akaionya isibweteke kwa kuidharau Yanga.

"Ukiangalia kikosi cha Simba ni kipana kina wachezaji wazuri wengi, hakitegemei mchezaji mmoja kuna kikundi cha wachezaji, ukiangali Luis Miquissone ambaye amekuja kuongeza nguvu tofauti na Yanga kumtegemea Bernard Morrison,"

"Ukiachilia Luis Simba kuna Clatous Chama nimeangalia mechi iliyopita [dhidi ya KMC FC] alitoa pasi muhimu na kuifanya wapate ushindi, lakini kuna Meddie Kagere, Deo Kanda, John Bocco na wengine wengi ni wazuri," alisema Talib na kuongeza:

# Rais CAF afuata dabi Simba, Yanga

**Na Somoe Ng'itu**

## ●●● Marefa watakaochezesha waonywa, wachezaji nao sasa kusalimiana 'ki-corona' staili ili...

HESHIMA ya mechi ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga inatarajia kuongezeka zaidi baada ya Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad kuwa miongoni mwa wageni watakaohudhuria mechi hiyo ya mzunguko wa pili inayotarajiwa kupigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

**Hii itakuwa ni mara ya tatu kwa kiongozi huyo wa CAF kuja nchini, lakini ni mara yake ya kwanza kushuhudia mechi hiyo inayovuta hisia za mashabiki wengi wa soka ndani na nje ya nchi.**

Taarifa zilizopatikana jijini jana zinaeleza kuwa Ahmad amethibitisha kuwa nchini na mbali na kushuhudia mchezo huo, pia atafanya mazungumzo na viongozi pamoja na wadau wa soka wa hapa nchini.

"Ndio anakuja nchini, ila kwa ufafanuzi zaidi, wasiliana na Rais wa TFF," alisema kiongozi mmoja wa TFF jina tunalihifadhi.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia alipoulizwa jana, aliliambia gazeti hili kuwa taarifa kamili kuhusiana na ujio wa kiongozi huyo wa juu katika medali ya soka barani Afrika ambaye ni raia wa Madagascar, itatolea rasmi leo.

"Naomba usubiri hadi kesho (leo), ndio tutatoa taarifa kamili kuhusiana na ujio wa Rais wa CAF, leo (jana) kuna habari mbalimbali, Simba na Azam wanacheza, Azam nao, na kuna habari nyingine," alisema kwa kifupi Karia.

Kwa mujibu wa taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jana, zinaeleza kuwa Ahmad atawasili nchini Jumamosi Machi 7 na kuondoka Machi 10, mwaka huu akirejea kwao Madagascar akipitia nchini Kenya.

Wadau mbalimbali waliozungumza na Nipashe kuhusu maoni yao ya mechi hiyo ya 'dabi' kuhudhuriwa na Rais wa CAF, walisema huu ni wakati wa mashabiki wengi kujitokeza kuujaza uwanja huo ili kumshawishi kiongozi huyo kuleta michuano mikubwa nchini.

Lakini walisema ni wakati wa waamuzi watakaopangwa kuchezesha mechi hiyo kuwa makini kwa kufuata sheria 17 za soka ili kudhihirisha ubora wa soka la Tanzania.

"Unajua kama tukijitokeza kwa wingi katika dabi hii, itamvutia kiongozi huyo na siku TFF ikiomba kuandaa michuano mikubwa CAF itashawishika kwa kuwa kuna mtaji wa mashabiki nchini," Mtanzania Ally Kimrume aliyeko Gaborone Botswana aliliambia Nipashe kwa njia ya simu baada ya kusikia taarifa za kiongozi huyo kuhudhuria mechi hiyo.

"Unajua kwa mfumo mpya wa michuano ya CAF ile ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, kwa sasa mechi ya fainali ni moja si nyumbani na ugenini tena, na nchi inayotaka ichezwe kwao, inatakiwa kuomba, hivyo bila CAF kujiridhisha inapochezwa kuna mtaji wa mashabiki wanaohudhuria uwanjani huwezi kupewa nafasi hiyo, hivyo dabi Jumapili ni wakati wa kuanza kujijengea msingi kwake," Kimrume aliongeza.

Collins Emily mdau mwingine wa soka, alisema: "Yale makosa ambayo yamekuwa yakifanywa na waamuzi wetu ni wakati wao wa kuongeza umakini, lakini wachezaji Simba na Yanga wanapaswa kuonyesha soka la kiwango cha juu na nidhamu ya mchezo maana uwapo wake uwanjani utafanya mechi hiyo kumulikwa na wageni wengi nje na ndani ya nchi."

Yanga ambao ndio wenyeji wa mchezo huo, watashuka uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya sare ya mabao 2-2 waliyopata katika mchezo uliopita, wakitokea nyuma na kusawazisha kupitia Mapinduzi Balama na Mohammed Issa 'Banka' huku yale ya Simba yakifungwa na Meddie Kagere na Deo Kanda.

Mechi hiyo ya watani pia inatarajiwa kutoa sura ya vita ya ubingwa wa msimu huu ambapo mpaka sasa bado ipo mikononi mwa vinara Simba, Azam FC, Yanga na Namungo ya mkoani Lindi.

Simba itashuka uwanjani ikiwa inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 65 (kabla ya matokeo ya mechi ya jana usiku dhidi ya Azam, FC), wakati Yanga yenye pointi 44 ina mechi mbili mkononi, wako katika nafasi ya nne.

**Wakati huo huo**, TFF imesema utaratibu wa wachezaji kusalimiana kabla ya kuanza kwa mechi hautatumika kwa sasa na badala yake watasalimiana kwa ishara tu.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema utekelezaji wa agizo hilo ulitarajiwa kutekelezwa kuanzia katika mechi zote zinazosimamiwa na shirikisho hilo kuanzia jana.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >